




UKURASA 3

**MAJERUHI** wa ajali iliyokatisha uhai wanafamilia watatu afariki dunia




UKURASA 13



# Nipashe

Jumamosi Desemba 3, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581148

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Wenye vyeti feki walipwa stahiki zao

UKURASA 2



Washtakiwa 11 wa mauaji ya mwanaharakati wa kupambana na ujangili, Wayne Lotter **(picha ndogo),** wakiwa kizimbani katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam jana, kabla ya kuhukumiwa adhabu ya kunyongwa hadi kufa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Wahukumiwa kunyongwa hadi kufa kumuua mwanaharakati wa tembo

UKURASA 2

UKURASA WA 3

## WANAWAKE WABAKWA NJIANI WAKIFUATA MAJI

BAADHI ya wanawake na wasichana wenye umri wa balehe katika Kata ya Lyamidati, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga wanadaiwa kukumbana na vitendo vya unajisi na ubakaji wakati wakitafuta maji. Vitendo hivyo vya kikatili vinadaiwa kufanywa na baadhi ya wanaume wakati...

UKURASA WA 4

## MWANAFUNZI ADAIWA KUUAWA KWA KUBAKWA

MWANAFUNZI wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi (FDC) Masasi mkoani Mtwara, Gloria Luoga (22) amekutwa ameuawa kinyama baada ya kudaiwa kubakwa na kundi la watu ambao hawajafahamika na mwili wake kutupwa...

## Utaratibu mpya matokeo NECTA wawaibua wadau

UKURASA 3

**MICHEZO** **POLISI TANZANIA YAIPANIA AZAM, YAMWAJIRI ZAHERA** UK. 28

**KATUNI** UK. 6




Wanafunzi wa Shule ya Msingi Mivumoni, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam, wakiwa wameshika mabango yenye ujumbe tofauti kuhusiana na ukatiliwa kijinsia, baada ya kupatiwa elimu hiyo na Shirika la Wanawake katika jitihada za kimaendeleo (WAJIKI), shuleni hapo juzi. **PICHA: PILLY KIGOME**

# Wenye vyeti feki walipwa stahiki zao

**Na Waandishi Wetu,**
ARUSHA

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) umewalipa wanachama 750 waliokumbwa na sakata la vyeti feki baada ya kuwasilisha madai yao na nyaraka stahiki.

Akizungumza wakati wa kikao kazi na wanachama wapatao 60 wa klabu ya waandishi wa habari Jiji la Arusha kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC) jana, Meneja Uhusiano na Elimu kwa Wanachama PSSSF, James Mlowe alisema ulipaji wa stahiki hizo kwa kundi hilo ulianza Novemba Mosi mwaka huu na ni endelevu.

"Zoezi linaendelea vizuri, wanachama waliopo katika orodha ya serikali na PSSSF ni 9,771 ambao wanadai malipo ya takribani Sh. bilioni 22.22," alifafanua.

Vilevile, alisema wanapitia madai ya wanachama wengine 2,800 waliokuwa wakiidai serikali Sh. bilioni 9.3 baada ya kuachishwa kazi kutokana na vyeti feki. "Ukijumlisha madai yote itakuwa jumla ya Sh. bilioni 31.56 kwa watu 12,666, hivyo tutatekeleza hivyo kama Rais Samia Suluhu Hassan alivyoagiza walipwe kwa kuwa wana mchango wao kwenye taifa hili," alisema.

Akizungumzia madhumuni ya kikao hicho na wanachama wa klabu hiyo ya waandishi wa habari jijini Arusha, Mlowe alisema ni kutoa ufafanuzi kuhusu utekelezaji wa majukumu ya mfuko pamoja na kuendeleza uhusiano mzuri uliopo kati ya mfuko na waandishi wa habari.

Mambo mengine aliyozungumzia Mlowe ni pamoja na malipo ya mafao na pensheni, uwekezaji, thamani ya mfuko pamoja na mafanikio ambayo PSSSF imeyapata tangu kuanzishwa kwake mwaka 2018 baada ya kuunganishwa kwa mifuko ya hifadhi ya jamii ya PSPF, PPF, LAPF na GEPF.

"Kila mwezi PSSSF inaingiza kwenye mzunguko zaidi ya Sh. bilioni 180 zikijumuisha malipo ya pensheni ya mwezi zaidi ya Sh. bilioni 60 zinazolipwa kwa wastaafu 158,000 pamoja na mafao mengine zaidi ya Sh. bilioni 120," alibainisha.

Mlowe alisema kuwa tangu kuunganishwa kwa mifungo hiyo mwaka 2018, wamepunguza gharama za uendeshaji kwa kiwango kikubwa.

"Kabla ya mifuko kuunganishwa matumizi yalikuwa ni Sh. bilioni 128 lakini baada ya kuunganishwa matumizi yamepungua hadi kufikia Sh. bilioni 67, hivyo tumeokoa Sh. bilioni 61," alifafanua.

Alisema thamani ya mfuko huo imepanda hadi kufikia Sh. trilioni 8.21 huku thamani ya uwekezaji katika miradi mbalimbali ya maendeleo ikifikia Sh. trilioni 7.52. Alisema thamani ya uwekezaji katika majengo imefikia asilimia 15 na uwekezaji wa amana za serikali kwenye benki ya kibiashara ni Sh. bilioni 400.

"Miezi mitatu tangu Rais Samia alipoingia madarakani alitoa hati fungani ya kulipa malimbikizo ya madeni kwa waliokuwa wanadai na sasa hivi hakuna tena malimbikizo," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya wanachama wenzake, Katibu wa Klabu hiyo, Seif Mangwangi alishukuru kwa fursa hiyo iliyowawezesha kufahamu kwa undani utekelezaji wa majukumu ya PSSSF na sasa wanaweza kutoa taarifa sahihi na muhimu kwa wadau wa mfuko huo.

**USULI**

Okotoba 26 mwaka huu, serikali kupitia kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, ilitangaza kurejesha michango ya watumishi 14,516 walioondolewa kwenye orodha ya utumishi wa umma baada ya kubainika kuwa na vyeti vya kughushi, ikitenga Sh. bilioni 46.8 kwa ajili ya kundi hilo.

Aprili 28 , 2016, Rais wa wakati huo, Dk. John Magufuli (Hayati) alikabidhiwa taarifa ya uhakiki wa vyeti vya watumishi wa umma mjini Dodoma na kuitaka Wizara ya Fedha na Mipango kuwaondoa kwenye orodha ya utumishi wa umma na kusimamisha mishahara ya waliobainika kuwa na vyeti vya kughushi.

Idadi yao iliyotajwa kipindi hicho ni 15,538 (walioondolewa kazini kwa kughushi vyeti au kutoa taarifa za uongo katika kumbukumbu zao rasmi za kiutumishi kuwa wana elimu ya kidato cha nne) pamoja na watumishi hewa 19,708, uamuzi uliotajwa kuiwezesha serikali kuokoa Sh. bilioni 19 kila mwezi.

# Wahukumiwa kunyongwa hadi kufa kumuua mwanaharakati wa tembo

**Na Grace Gurisha**

WATU 11 wakiwamo raia wawili wa Burundi katika kesi ya mauaji ya mwanaharakati mpinga ujangili dhidi ya tembo, Wayne Lotter (52), raia wa Afrika Kusini, wamehukumiwa kunyongwa hadi kufa baada ya kupatikana na hatia ya kuua kwa kukusudia.

Washitakiwa hao ni Rahma Mwinyi, Godfrey Salamba, Chambie Ally, Allan Mafue, Ismail Mohamed, Leonard Makoi, Ayoub Kiholi, Michael Kwavava na raia wa Burundi, Habonimana Nyandwi na Nduimana Ogiste.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Jaji Leila Mgonya wa Mahakama Kuu, Kanda ya Dar es Salaam baada ya upande wa Jamhuri kuthibitisha mashtaka bila kuacha shaka yoyote kwamba washtakiwa walimuua Lotter kwa kukusudia na kwa maslahi yao jambo ambalo ni kinyume cha sheria.

Akitoa hukumu hiyo, Jaji Mgonya alisema upande wa Jamhuri ulithibitisha kesi hiyo kwa kuleta mashahidi 32 na vielelezo 43, ambavyo vimethibitisha bila shaka kuwa washtakiwa walitenda kosa hilo.

Jaji Mgonya alisema Katiba ya nchi inaelezea kuishi ni haki ya kila mmoja na ndiyo haki mama na hakuna yeyote anayeruhusiwa kutoa uhai wa mtu mwingine kwa ajili ya maslahi yake.

Pia alisema uhai wa mtu ni kitu kitakatifu ambapo katika kesi hii inajumuisha watu walioutoa uhai wa mtu ambae hana hatia na aliyekuwa anatetea rasilimali za Tanzania.

Jaji alisema kutokana na kosa walilolitenda washtakiwa hao kumuua mtu asiye na hatia Mahakama inawatia hatiani pamoja na kuhukumiwa kunyongwa hadi kufa na rufani iko wazi endapo hawajaridhika na hukumu hiyo.

Kabla ya jaji kusoma hukumu hiyo, Wakili wa Serikali Mkuu, Yamiko Mlekano, aliiomba mahakama kutoa kibali cha kuteketezwa baadhi ya vielelezo kwa kuwa ni hatari kuvihifadhi huku akiomba kutaifishwa baadhi ya vielelezo ambavyo vimetumika katika ushahidi.

Alidai vielelezo hivyo ni bomu la kurushwa kwa mkono, bunduki mbili, maganda ya risasi na risasi ambavyo vinahitaji kuteketezwa huku magari mawili aina ya Toyota IST na Toyota Sienta moja ambavyo yanatakiwa kutaifishwa kuwa mali ya Serikali.

Hata hivyo, wakili wa utetezi, Mluge Kaloli, alidai hana kipingamizi juu ya uteketezwaji wa silaha hizo lakini akaomba magari aina ya IST pamoja na kadi yarudishwe kwa wenyewe kwa sababu waliachiwa huru na mahakama kuwa hawana kesi ya kujibu.

Mlekano alipinga hoja hiyo kuwa hakuna shaka mshitakiwa aliachiwa lakini gari lake lilitumika kutenda uhalifu, hivyo Jaji akakubaliana na hoja hiyo na kutoa amri kuwa magari hayo yataifishwe na vielelezo hivyo kuteketezwa.

Washtakiwa wote 11 wanadaiwa walifanya kikao na kukubaliana kununua silaha kutoka Burundi kwa ajili ya kumuua Lotter na ilisafirishwa isivyo halali na kuingia nchini.

Ilidaiwa kuwa kati ya Julai Mosi na Agosti 16, 2017, washtakiwa wakiwa maeneo ya Dar es Salaam na Arusha walikula njama ya kutenda kosa la mauaji dhidi ya Lotter.

Ili kutekeleza huo mpango, walidaiwa kufanya kikao na kukubaliana kununua silaha kutoka nje ya Tanzania na Fahame Karama ambaye hajapatikana hadi sasa alichukua Sh. milioni tatu na kumpatia Makoi ambaye alimtumia Nduimana kwa njia ya Western Union kwa ajili ya kununua silaha nchini Burundi.

Nduimana anadaiwa alinunua silaha hiyo aina ya UZI na risasi 200 kisha aliisafirisha isivyo halali kuingia Tanzania akawakabidhi Karama na Mwinyi. Lotter alikuwa Mkurugenzi na Mwanzilishi-Mwenza wa Shirika lisilo la kiserikali la PALMS Foundation.

Awali, kesi hiyo ilikuwa na washitakiwa 22 na hadi kumalizika, washitakiwa waliobaki na kuhukumiwa kunyongwa hadi kufa ni 11, wanne waliondolewa na Jamhuri na saba waliachiwa baada ya kuonekana hawana kesi ya kujibu.

Hukumu hiyo ilisomwa kuanzia saa 4:54 asubuhi na kumalizika saa 7:48 mchana na ambapo baada ya hukumu hiyo, Rahma ambaye ni mwanamke peke yake kwenye kesi hiyo, alikuwa akilia huku baadhi ya ndugu na jamaa na wao wakilia kwa kutokuamini kilichotokea.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa kwa pamoja wanadaiwa kati ya Julai Mosi na Agosti 16, 2017 walikula njama ya kufanya mauaji dhidi ya Lotter.

Katika shtaka la pili, washtakiwa wanadaiwa Agosti 16, 2017 katika makutano ya barabara za Chole na Haile Selassie, wilayani walimuua Lotter ambaye alikuwa mwanaharakati wa kupambana na mauaji ya Tembo.

# Wanawake wanabakwa njiani wakifuata maji

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

BAADHI ya wanawake na wasichana wenye umri wa balehe katika Kata ya Lyamidati, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga wanadaiwa kukumbana na vitendo vya unajisi na ubakaji wakati wakitafuta maji.

Vitendo hivyo vya kikatili vinadaiwa kufanywa na baadhi ya wanaume wakati wanawake hao wakitembea umbali wa zaidi ya kilometa 15 kusaka maji katika kata ya jirani ya Lyabukande.

Kata hiyo yenye jumla ya vijiji sita, inebainishwa kuwa viwili vya Katodo na Kizungu vina maji ya kutosha wakati vijiji vilivyobaki vya Mwabasi, Lyamidati, Ihugi na Bukiligulu hutumia maji ya visima vifupi ambavyo wakati wa kiangazi hukauka na wanakijiji kulazimika kutembea umbali huo kuyatafuta.

Nipashe ilipewa taarifa hizo jana wakati wa utekelezaji wa Mradi wa Sauti za Kaya na Vyombo vya Habari katika kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto unaotekelezwa na Klabu ya Waandishi wa Habari mkoani Shinyanga (SPC) kupitia Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT).

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Tanganyika Senta, Ramadhani Juma alisema wanawake wengi wamekuwa wakikumbwa na vitendo vya ubakaji wakiwa njiani kutafuta maji katika kata ya jirani.

Alisema licha ya ukatili huo kufanyika dhidi yao, wengi wao hushindwa kutoa taarifa kutokana na kutishiwa kurogwa baada ya kufanyiwa ukatili huo.

Alisema watuhumiwa hao wamekuwa wakitumia nafasi ya kufanya vitendo hivyo pindi baiskeli ambazo wanawake hutumia kusafirisha madumu yenye maji, zinapoharibika njiani, huwavamia na kufanyiwa ukatili huo.

"Mradi wa bomba la Ziwa Victoria umepita wenye kata yetu na kuelekea mkoani Tabora, wao wanakunywa maji wakati sisi tunayakosa, wake na watoto wetu wanaendelea kubakwa wakisaka maji, tunawaomba viongozi watusaidie angalau watueletee maji safi ili kuondokana na ukatili huu kwa wanawake," alisema.

Sofia Boniphace alilitaja tukio lililotokea mwaka jana la mtoto wa kike ambaye alinajisiwa lakini wazazi wake walishindwa kutoa taarifa ofisi ya kata badala yake familia za pande mbili zilikutana na kumalizana kwa kupeana fedha.

Ofisa Maendeleo ya Jamii, Irene Mchuma alikiri kuwapo kwa matukio ya hayo lakini wananchi hushindwa kuwapa taarifa kutokana na vitisho.

Alisema katika kutokomeza vitendo hivyo wamekuwa wakipita ndani ya jamii na kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia.

Alitoa mfano wa mama ambaye alibakwa na kutoa taarifa katika ofisi hiyo lakini wakati ufuatiliaji ukiendelea, mwanamke huyo alirudi ofisini hapo kuomba mtuhumiwa asichukuliwe hatua na walipogoma, alihama na haijulikani aliko.

Sera ya Maji inayotekelezwa kwa sasa nchini, pamoja na mambo mengine, inataka serikali kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama ndani ya mita 400 kutoka kwenye makazi yao.

# Wadau wafunguka utaratibu mpya wa matokeo NECTA

**Na Romana Mallya**

WADAU wa sekta ya elimu wameunga mkono mfumo mpya wa utangazaji wa matokeo ya mtihani bila kutaja shule bora na wanafunzi bora, wakisema utaratibu huo ulikuwa unachangia kuwapo vitendo vya udanganyifu.

Ni kauli waliyoitoa jana muda mfupi baada ya Baraza la Mitihani (NECTA) kutangaza matokeo ya mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi (PSLE) kwa mwaka 2022 bila kuwapo shule bora kitaifa na wanafunzi bora kitaifa wala shule zilizofanya vibaya kama ilivyozoeleka awali.

Mkuu wa Miradi wa Taasisi ya HakiElimu, Godfrey Bonaventure alisema wanaungana na NECTA katika hilo, akisisitiza hakuna haja kutangaza nani amekuwa wa kwanza au wa mwisho.

"Huo ni mchakato wa ndani, kutangaza shule hii imekuwa ya mwisho, umekuwa ni changamoto na kusababisha shule kupambana kwa namna yoyote ili isiwe ya mwisho, na 'ndo' (utaratibu) ulikuwa unasababisha udanganyifu unakwenda huko.

"Badala ya kujikita kufundisha watoto, unakuta Mkuu wa Wilaya anatoa matamko 'sitaki kuona wilaya yangu imekuwa ya mwisho' na kushushana vyeo.

"Kusema shule ya kwanza au ya pili, tunamaanisha kwamba shule ni biashara na shule zimekuwa zikitumia nafasi hiyo kujikita zinafanya za juu ili kuvutia wateja. Imefika mahali ukipita barabarani unaona basi la shule limeandikwa namba moja kimkoa, hii inamaanisha nini?" alihoji.

Alisema sekta nyeti ya elimu lazima ijikite kwenye mukhtadha wa kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia ili watoto wapate elimu bora, akiwasilisha hoja "kwanini katika taasisi za elimu ya juu huwa hawatangazi chuo cha bora na kisicho bora?"

"Tutambue shule kwa kuweza kufaulisha kwa wastani A au B kuliko kujikita kwenye namba moja au namba mbili, tunataka kuwapo ufaulu wa pamoja," alisema.

Mdau wa mwingine wa elimu, Mark Masangya alisema wamefurahishwa kwa kuwa kilichofanywa na NECTA ndicho kinachopaswa kufanyika kwa miaka mingi iliyopita kwa kuwa matokeo yanatakiwa yaheshimike na yasifanywe biashara.

"Mpaka kufikia hapo changamoto tulizopitia kama wadau ni watu kushindana kwa kutumia mbinu ambazo siyo nzuri na ndiyo maana unakuta wengine wamefutiwa matokeo yao, huu ndiyo mtazamo mzuri na unapaswa kuendelezwa," alipongeza uamuzi wa NECTA.

Mwenyekiti wa Taifa wa Shirikisho la Wamiliki wa Shule na Vyuo Binafsi Tanzania (TAMONGSCO), Leonard Mao, alisema: "Kama NECTA imeamua kuondoa mfumo huo, ni sawa kwa kuwa ule ushindani katika ya shule za serikali na binafsi nao utakuwa umeondoka."

**WAZAZI WAFUNGUKA**

Mkazi wa Temeke mkoani Dar es Salaam, Suleiman Ally pia aliipongeza NECTA kwa kubadilisha mfumo wa utangazaji wa matokeo, akisisitiza kuwa uliokuwapo ulikuwa unatumika kuzitangaza shule fulani na kusababisha baadhi kutumia kigezo hicho kupandisha ada.

Mkazi wa Mwenge mkoani Dar es Salaam, John Mwaipopo alisema mfumo huo mpya utaleta usawa na kuondoa hofu kwa watoto katika ushindani.

Anna Stanslaus, mkazi wa Mwananyamala wilayani Kinondoni, alisema mfumo huo mpya hauna afya katika sekta ya elimu kwa sababu hata katika michezo ushindani ni lazima.



Daladala lenye namba za usajili T 944 DHB, linalofanya safari zake kati ya Mloganzila na Makumbusho, likiwa limepata ajali baada ya kumshinda dereva wake na kutumbukia kwenye mfereji wa maji ya mvua katika Barabara ya Bagamoyo, eneo la kituo cha basi cha ITV Mwenge, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Majeruhi ajali iliyokatisha uhai wanafamilia watatu afariki dunia

**Na Romana Mallya**

KIJANA Albert Mrema aliyelazwa kwa siku saba kwenye Chumba cha Uangalizi Maalum (ICU) katika Hospitali ya Mlongazila mkoani Dar es Salaam baada ya ajali iliyosababisha familia ya watu watatu kupoteza maisha, amefariki dunia usiku wa kuamkia jana.

Ajali hiyo ilitokea Jumamosi iliyopita eneo la Kibamba Hospitali mkoani Dar es Salaam wakati familia hiyo ikitoka Kibaha mkoani Pwani kwenye mahafali ya kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Gili. Waliofariki dunia dunia kutokakana na ajali hiyo na kuzikwa juzi ni Immaculata Byemerwa (mama) na wanawe, Janeth Byemerwa aliyekuwa mwanafunzi wa mwaka wa tatu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) akisomea Uhandisi Ujenzi (Bsc.Civil Engineering) na Jollister Byemerwa aliyehitimu kidato cha nne mwaka huu, wakimwacha Albert akiwa majeruhi.

Katika ajali hiyo, Albert ndiye alikuwa dereva wa gari lenye namba za usajili T 597 BWU aina ya Toyota Prado ambalo wakati likitoka Kibaha kuelekea Tabata nyumbani kwao na baada ya kufika hapo liliacha njia na kuingia bondeni.

Kaka wa marehemu Immaculata, Patrick Mpocholwa aliithibitishia Nipashe jana kuwa Albert ambaye alikuwa akipigania uhai wake hospitalini Mloganzila, naye alifariki dunia usiku wa kuamkia jana majira ya saa nane.

"Albert ambaye alikuwa amelazwa ICU Mlongazila amefariki dunia usiku wa kuamkia leo (jana) majira ya saa nane, tunaomba mwendelee kutuombea," alisema.




Meneja wa Fedha wa Benki ya KCB, Goodluck Alphonce (wa pili kulia), akipokea tuzo kutoka kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Mipango na Fedha) Ikulu Zanzibar, CPA Jamal Kassim Ali, kwa ushindi wa nafasi ya pili katika umahiri wa uandaaji wa mahesabu kwa mwaka 2021, zilizotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA), mkoani Dar es Salaam mapema wiki hii. Kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya NBAA, CPA Silvia Temu na (kulia) ni Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani wa KCB, Magreth George. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mwanafunzi adaiwa kuuawa kwa kubakwa

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MWANAFUNZI wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi (FDC) Masasi mkoani Mtwara, Gloria Luoga (22) amekutwa ameuawa kinyama baada ya kudaiwa kubakwa na kundi la watu ambao hawajafahamika na mwili wake kutupwa kwenye kichaka.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Rest Camp, Kata ya Mkomaindo, Zainab Nachungu, akizungumza jana eneo la tukio, alisema tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia juzi na kwamba taarifa za kuonekana kwa mwili wa mwanafunzi huyo, zilianza kuzagaa majira ya saa 12:00 juzi asubuhi baada ya wapita njia kuuona ukiwa kichakani.

Alisema wahusika wa mauaji hayo baada ya kufanya hivyo, waliutupa mwili wa binti huyo katika kichaka kilichoko karibu na Shule ya Msingi Mkomaindo ukiwa umeachwa utupu.

Nachungu alisema uongozi wa serikali ya Mtaa kwa kushirikiana na uongozi wa kata, ulifika sehemu ya tukio mwili wa mwanafunzi ulipokuwa umetupwa.

Alisema wasamaria wema ambao walikuwa wameuona mwili huo, walitoa taarifa kwenye uongozi wa serikali ya mtaa na baada ya hapo uongozi ulibaini kuwa mwili huo ni wa mwanafunzi na hatimaye kutoa taarifa kituo cha polisi Masasi.

Baada ya kupokea taarifa, alisema polisi walifika sehemu ya tukio na kuuchukua mwili huo na kwenda kuuhifadhi katika chumba cha kuhifadhia maiti katika Hospitali ya Mji wa Masasi Mkomaindo.

"Uongozi wa serikali ya mtaa kwa kushirikiana na uongozi wa kata ya Mkomaindo, tumeshawafahamu wazazi wa binti huyo na taratibu za kuwakabidhi mwili zinaendelea kufanyika. Lakini kipekee tunasikitishwa na matukio ya mauaji ya wasichana yanayofanyika wilayani Masasi. Tunaiomba serikali iendelee kuchukua hatua ili kukomesha matukio haya," alisema.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Mkomaindo, Dk. Catherine Paschal, alikiri kupokea mwili wa mwanafunzi huyo juzi majira ya saa 4:00 asubuhi na baadaye waliufanyia uchunguzi wa kitabibu na matokeo ya uchunguzi yalionyesha aliingiliwa na wanaume au kubakwa na kundi la watu.

Alisema uchunguzi huo pia ulibaini kuwa binti huyo kabla ya kuingiliwa, alikosa hewa na huenda hicho pia ni chanzo kingine cha kumfanya kupoteza maisha na kwamba mdomoni alikuwa akitokwa na mapovu.

Baba mzazi wa mwanafunzi huyo aliyejitambulisha kwa jina moja la Luoga, alisema amepokea kwa masikitiko taarifa za mwanawe kuuawa kinyama na kwamba amepoteza mtoto ambaye alikuwa ana matarajio naye.

Alisema alipigiwa simu ya kupewa taarifa ya mtoto wake kuokotwa akiwa ameuawa huku akidaiwa kubakwa akiwa kijijini ambako alikwenda kufanya kazi zake za ujenzi na baada ya taarifa hizo alilazimika kurudi nyumbani kwa ajili ya taratibu zingine za kifamilia.

"Kwa kweli nimeumizwa sana juu ya kifo cha mwanangu kwa kuuawa kinyama. Siku zote nilikuwa ninamsihi juu ya usalama wake kwani matukio kama haya kwa sasa Masasi yamekuwa ya mara kwa mara. Tunaiomba serikali idhibiti matukio haya," alisema.

Mkuu wa FDC, Sophia Mkopi, alipohojiwa na Nipashe ofisini kwake, alikiri kuwa binti huyo ni mwanafunzi wa chuo hicho na kwamba takribani wiki moja alikuwa hajafika chuoni.

Alisema mwanafunzi huyo alikuwa akisoma kwenye chuo hicho fani ya ushonaji na alikuwa akisoma kwa ufadhili wa serikali kupitia programu maalumu ya miezi sita ambayo inasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Watu Wenye Ulemavu na alitarajia kuhitimu mwezi huu.

Mkopi alisema uongozi wa chuo umepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kuuawa kwa mwanafunzi huyo na kwamba utashirikiana bega kwa bega na familia ya marehemu katika kuhakikisha shughuli za kuuhifadhi mwili huo zinakwenda vizuri.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Lucas Katembo, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba uchunguzi wa kipolisi juu ya tukio hilo unaendelea ili kuhakikisha wahusika wanakamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

## Makali mgawo wa umeme yapungua

**Na Maulid Mmbaga**

JITIHADA za Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) za kupunguza mgawo wa umeme zimeendelea kuzaa matunda baada ya kukamilika kwa matengenezo ya mitambo ya kuzalisha nishati hiyo.

Matengenezo hayo yamesaidia kuongezeka kwa kiwango cha umeme kutoka upungufu wa megawati 300 wiki iliyopita hadi 210.

Akitoa taarifa ya hali ya umeme jana Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande, alisema uzalishaji wa umeme umeongezeka baada ya kukamilika kwa matengenezo katika mtambo wa Ubungo III ambao umeingiza megawati 35 kwenye gridi ya taifa.

Chande alisema jitahada hizo zimefanikisha pia kukamilika kwa mtambo wa Kinyerezi II ambao unazalisha megawati 215 na Kidatu ambao unatoa megawati 50 na kwamba zote zimeshaingia kwenye mfumo.

Hata hivyo, alisema kuna baadhi ya maeneo bado uzalishaji wa nishati hiyo haujapanda kutokana na kina cha maji kuwa kidogo.

"Tumeona mvua zimeanza kunyesha lakini zinazotusaidia sisi ni zinazonyesha katika mikoa ya Morogoro, Iringa, Njombe na Dodoma ambazo zinasaidia kujaza maji kwenye mabwawa ya kuzalisha umeme ya Mtera, Kihansi na Kidatu. Katika maeneo hayo bado hatujaona mtiririko wa maji ya kutosha kuongeza uzalishaji.

"Kutokana na hali hiyo, tumeelekeza nguvu kubwa kwenye uzalishaji wa umeme kwa kutumia gesi na jua. Lazima tuwe na vyanzo mbalimbali vya kuzalisha nishati, hatuwezi kutegemea chanzo kimoja. Vyanzo tofauti vinatumika ili kuwe na uhakika wa umeme na hii itasaidia muda wa saa za umeme kukatika kupungua," alisema Chande.

Aidha, Chande alisema wanaendelea na majaribio ya mitambo miwili katika kituo cha upanuzi cha Kinyerezi I ambayo inaingiza megawati 65 katika gridi ya taifa huku akibainisha kuwa wanatarajia hadi kufikia mwishoni mwa mwezi huu, mitambo hiyo itakuwa inazalisha megawati 90.

Pia alisema bado wanaendelea na kazi ya matengenezo ya mitambo miwili ya Ubungo III ambayo inatarajiwa itakamilika mwishoni mwa mwezi huu na kuzalisha megawati 40.

Sambamba na hayo, alisema wanatarajia mitambo mingine miwili kuanza kufanya kazi katika kituo cha upanuzi cha Kinyerezi I kuanzia Februari, mwakani ili kuingiza megawati 90 kwenye gridi ya taifa.

"Iwapo mvua zitaendelea kunyesha katika mabwawa yote ya kuzalisha umeme na matengenezo yaliyobakia kukamilika kama ilivyopagwa, tunategemea hali ya umeme itaendelea kuimarika na tunatarajia upungufu wa umeme kwa siku kuendelea kupungua," alisema.

"Wakati kazi zote hizi zikiendelea kufanyika, shirika litaendelea kutoa taarifa na ratiba ya upungufu wa umeme kadri inavyozidi kuimarika," aliongeza.

# Makamu Rais ahimiza ulinzi wa bahari, kitaifa na kikanda

**Na Jenifer Gilla**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla amesema ili kupata matokeo mazuri kwenye ulinzi wa bahari, kunahitajika ushirikiano wa kitaifa na kikanda kwa kuwa hakuna nchi inayoweza kufanya jambo hilo peke yake.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano uliokuwa ukijadili hali ya usalama wa bahari ulioandaliwa na Kituo cha Sera za Kimataifa Afrika (CIP) ambao taasisi za kitaifa na kimataifa zinazohusika na uchumi wa bahari zilihudhuria.

Abdulla alisema ukanda huo una kikwazo cha kutokuwa na sera za muda mrefu za usalama wa bahari, hali iliyosababisha kesi zinazohusu bahari kushughulikiwa kwa njia za kawaida na kuchochea kuwapo vitendo vya uhalifu.

Alisema Tanzania bado ina kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha bahari pamoja na wanufaika wake wanakuwa salama ikiwamo upatikanaji wa vifaa salama, elimu na utaalamu.

"Tukishirikiana kwa pamoja tunaweza kufika pale ambapo tumekusudia, maana ukanda huu ni mkubwa, kuna nchi nyingi zinahusika," alisema.

Abdulla alisema mkutano huo ni muhimu kwa kuwa bahari inapitia vitisho vingi vikiwamo vitendo vya ujambazi, ugaidi, ulanguzi wa uharamia wa mihadarati, bidhaa zisizofaa, kuenea kwa silaha, uvuvi haramu, uhalifu wa kimazingira, ajali na majanga.

"Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na ugunduzi mkubwa wa mafuta na gesi katika ukanda wa bahari ya Afrika na Mashariki, ugunduzi huu hutoa uhakika wa usalama wa nishati kwa jamii na eneo pana," alisema.

Aliahidi kuwa maazimio ya mkutano huo yatafanyiwa kazi na serikali kwa kushirikiana na wadau wengine wa bahari ambao wameonyesha nia kubwa ya ushirikiano katika kuhakikisha kunakuwa na salama ili kukuza uchumi wa bluu.

Rais wa CIP, Omega Mjenga alisema kituo hicho kinaendelea kushirikiana na serikali katika kuhakikisha kunakuwa na usalama wa bahari.

Aliwataka wadau wengine waendelee kujitokeza kushirikiana nao katika maeneo sita wanayoyafanyia kazi ambayo ni ulinzi na usalama na sera za kigeni na ufanyaji uamuzi.

Mengine aliyotaja ni demokrasia na utawala wa kimataifa, wanawake, jinsia na makundi yaliyotengewa nishati, mazingira na usalama wa chakula na sera za uchumi za kimataifa.

## Vijana wanolewa kukabili mabadiliko ya tabianchi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

JUKWAA la Mabadiliko ya Tabia ya Nchi (FORUMCC), limeanza kutoa mafunzo kwa vijana na asasi za kiraia katika wilaya nne ikiwamo ya Singida ya jinsi ya kutekeleza mradi wa ushirikiano wa kimkakati (SPAII) unaolenga kujenga uhimilivu dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi.Ofisa Programu wa FORUMCC, Msololo Onditi, akizungumza jana katika mafunzo hayo ambayo yameanza kwa vijana 25 wa wilaya ya Singida, alisema mradi huo unatekelezwa kwa kushirikiana na Shirika la Action Aid Tanzania kwa ufadhili wa Action Aid Denmark.

Alisema mradi huo ambao ni wa kimkakati, umeanza kutekelezwa mwaka huu katika wilaya za Kusulu na Kibondo mkoani Kigoma, Singida na Tanga huku walengwa wakuu wakiwa vijana hususani wasichana.

Onditi alisema mradi huo unalenga kupunguza athari za kimazingira kwa vijana hususani katika maeneo yanayopokea wakimbizi na kuhakikisha vijana wananufaika na uwajibikaji wa viongozi wa umma katika mipango na maandalizi ya bajeti kwa mlengo wa kijinsia na haki za kidemokrasia.

Katika mafunzo hayo, mada zinazojadiliwa ni maana ya mabadiliko ya tabia ya nchi na vyanzo vyake, kuhimili na kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Mada nyingine ni upotevu na uharibifu unaosababishwa na mabadiliko ya tabia ya nchi na mfumo wa kitaasisi kuhusu upatikanaji wa fedha za mabadiliko tabia ya nchi kidunia. Pia lengo kuu la mafunzo ni kuwajengea vijana na asasi za kiraia uwezo wa kuchagiza ubunifu wa vyanzo vya fedha ili kuwezesha jitihada za kuhimili athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Alisema mradi huo unatekelezwa kutokana na ukweli kwamba utegemezi mkubwa kwa fedha za wafadhili unaathiri jitihada za ndani na wakati athari za mabadiliko tabia nchi zinaendelea kukua mwaka hadi mwaka.

Nao washiriki wa mafunzo hayo walisema mkoa wa Singida uko hatarini kuendelea kukumbwa na mabadiliko ya tabianchi, hivyo zinahitajika jitihada za makusudi ili kuinusuru jamii na vizazi vijavyo.

Walisema kuwa tozo mbalimbali za mazao ya kilimo na miamala ya simu zinaweza kuwa vyanzo vya mapato ya fedha za kukabili changamoto za mabadiliko ya tabia nchi.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Usajili wa dirisha dogo ufanyike kwa malengo

**SHIRIKISHO** la Soka Tanzania (TFF), limetangaza kufungua dirisha dogo la usajili wa wachezaji litakaloanza ifikapo Desemba 16, mwaka huu na litamalizika ifikapo Januari 15, 2023.

Usajili huo utazihusu tu timu ambazo hazikuwa zimekamilisha idadi kamili ya wachezaji 30 ambao iliwanasa katika dirisha kubwa la usajili lililopita, hivyo wanalazimika kuongeza nguvu ili kujiweka katika nafasi nzuri zaidi.

Pia itazingatia idadi ya wachezaji wa kigeni ambao wanahitajika kwa mujibu wa kanuni, inafahamika msimu huu wa 2022/2023, timu zimeruhusiwa kusajili wachezaji kutoka mataifa mengine wasiozidi 12.

Dirisha dogo linawahusu wamiliki wa timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi ya Championship zamani Ligi Daraja la Kwanza na First League (Ligi Daraja la Pili), ligi hizi zote zinakaribia kukamilisha mzunguko wake wa kwanza hivi karibuni.

Lakini inaweza pia kuwa faraja kwa timu zinazoshiriki Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania kukamilisha mapungufu ambayo imeyabaini baada ya kucheza michezo mbalimbali ya kirafiki kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya wa ligi hiyo unaotarajiwa kufanyika kuanzia Desemba 6, mwaka huu.

Mchakato huu utaonekana bora au wenye tija kwa timu zote endapo viongozi wa timu husika watashirikiana vizuri na makocha ili kukamilisha usajili huo na hatimaye malengo yaliyowekwa na klabu husika yakafikiwa.

Tunawakumbusha mapendekezo kutoka kwa makocha ndiyo yanatakiwa kufanyikwa kazi na endapo timu itasajili wachezaji wapya kwa kukurupuka, basi usajili huo hautawasaidia na matokeo yake watashindwa kufikia malengo ya kutwaa ubingwa kwa walioko kwenye mbio hizo au wale wanaohitaji kujinusuru na janga la kushuka daraja wanaweza kubakia mkiani.

Ni mapema kuzungumzia timu inayoweza kutwaa ubingwa katika ligi zote zinazoendelea kwa sasa nchini, lakini dalili njema ya timu kupata matokeo chanya huanzia kwa kila kiongozi kutekeleza majukumu yake.

Timu ambayo itaamua kufanya usajili wa dirisha dogo bila kufuata mapendekezo ya kiufundi, ni sawa na timu itakayochagua kujichimbia mkiani kwenye ligi badala ya kusajili wachezaji watakaoongeza nguvu na kutoka pale walipo, na kwenda kwenye daraja la juu.

Ukiondoa suala la timu kusajili nyota wapya, huu ni wakati mwingine wa wachezaji ambao wamekosa namba kwenye klabu walizopo kuomba ruhusa ya kwenda kusaka changamoto nyingine, na hii si tu itasaidia kumjenga mchezaji husika, lakini huenda ikafungua milango ya mafanikio ambayo ilisimama.

Mchezaji anatakiwa kutoweka maslahi ya fedha mbele, kuna wakati kulingana na umri, anatakiwa kuhakikisha analinda kipaji chake kwa kukubali kusajiliwa na timu itakayompa nafasi ya kucheza na si kubakia kuonekana mazoezini au kwenye mechi za kirafiki.

Ni kweli inahitaji kufanya uamuzi mgumu wa kutoangalia fedha, lakini ikumbukwe kucheza mpira ndio kazi yako, na kama fursa hiyo haipatikani, basi ni vizuri kuchekecha ubongo na kuchagua jambo litakalokuwa na afya kwenye taaluma hiyo ambayo ameichagua.


Ili yote haya yafanyike, Idara ya Ufundi ya TFF iliyoko chini ya Mkurugenzi, Oscar Mirambo, inatakiwa kukaa karibu na wachezaji ambao inawafahamu wako kwenye timu ambayo ni wazi kupata namba katika kikosi cha kwanza ni vigumu, wakapata ruhusa ya kwenda kuboresha viwango vyao kwingine na kukawekwa makubaliano rasmi ya kurejea endapo wataimarika.

Kufanya hivi si tu kutasaidia kuwajenga wachezaji ambao baadhi yao makazi yao ya kudumu ni benchi, lakini itakuwa ni kuwapa fursa nyota hao kujiimarisha na baadaye kuitwa katika timu za taifa, kwa sababu idadi kubwa ya wanaokaa benchi ni wachezaji wazawa.

Ifike wakati hata mchezaji husika akawa huru kuomba baraka za timu yake kwenda kujiunga katika timu nyingine ili kujiimarisha na kuacha kuangalia maslahi ya fedha peke yake huku kipaji chake kikiendelea kuzama.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Yanga ilijipa yenyewe presha ya 'Unbeaten'

**HAKUNA** shabiki yeyote wa soka nchini aliyetegemea Yanga ingeshindwa kuendeleza mechi zake mfululizo za kucheza bila kupoteza pale ilipokutana na Ihefu SC.

Inawezekana wapo waliotarajia Yanga inaweza kupoteza mechi msimu huu tofauti na msimu uliopita, lakini siyo na timu hiyo yenye makazi yake Mbarali, mkoani Mbeya.

Wengi walitarajia kama ni kupoteza, basi inaweza kupoteza dhidi ya timu mbili kubwa ambazo ni Simba au Azam FC, kwenye mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Msimu uliopita Yanga ilicheza mechi zote za msimu bila kupoteza. Ilicheza mechi 30, ikishinda 22, sare nane, ikavuna pointi 74, lakini msimu huu imecheza mechi 12. Kati ya mechi hizo ikashinda 10 na sare mbili, kabla ya kupoteza kwenye mechi ya 13.

Mara ya mwisho Yanga kupoteza kabla haijapoteza dhidi ya Ihefu ilikuwa ni Aprili 25, 2021 kwenye mzunguko wa pili wa Ligi Kuu 2020/21 na baada ya hapo ikacheza mechi 49 bila kupoteza.

Tayari klabu hiyo imetangaza kufanya sherehe ya kucheza idadi hiyo ya mechi bila kupoteza itakayofanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kesho wakati timu hiyo itakapowakaribisha Prisons.

Itapambwa na burudani kutoka kwa wasanii mbalimbali wa hapa nchini.

Baada ya kupoteza bila kutegemea, kumekuwa na sababu mbalimbali ambazo zimetolewa nba benchi la ufundi pamoja na baadhi ya viongozi zilizosababisha timu hiyo ipoteze, tena na timu ambayo mpaka inacheza nayo mechi hiyo ilikuwa inaburuza mkia.

Uchovu wa wachezaji ulikuwa ni namba moja, yaani wachezaji wa timu hiyo wamecheza mechi nyingi sana mfululizo, za ligi pamoja na za kimataifa.

Pili baadhi ya wachezaji pia walikuwa wakicheza wakiwa majeruhi. Kocha Msaidizi, Cedric Kaze, alisema kwenye mechi hiyo ilifika wakati wachezaji walionekana wazito kukimbia.

Tunakubali kwa sababu zote hizo ni za kiufundi. Binafsi nikiangalia ni Yanga ilionekana kabisa inakwenda kumaliza 'Unbeaten' zake kadri siku zilivyozidi kusonga mbele.

Ingeweza kupoteza 'Unbeaten' hiyo tangu kwenye mechi dhidi ya Kagera Sugar iliyofanyika Novemba 13, mwaka huu lakini ikashinda bao 1-0. Ni mechi ambayo Kagera Sugar ilicheza vyema zaidi kuliko Yanga, ikikosa penalti na nafasi nyingi za kufunga.

Dodoma Jiji nayo ingekuwa makini kutumia nafasi ingeweza kuifunga Yanga, mechi iliyochezwa Novemba 22, mwaka huu. Ni mechi ambayo Dodoma Jiji ilikosa mabao mengi zaidi ya wazi na mwisho wake ilichapwa magoli 2-0.

Hizi ni mechi ambazo Yanga ilipotea chupuchupu kupoteza 'unbeaten' yake, lakini ilisalimika kwa kutokuwa makini kwa timu ilizocheza nazo.

Ni wazi wachezaji wa Yanga hawakuonekana kucheza kwenye kiwango chao cha kawaida, niseme tu Yanga ingeweza kucheza mechi hata 60 za Ligi Kuu, lakini haikufanikiwa kwa sababu pamoja na matatizo yaliyoanishwa lakini ilianza kujitia presha yenyewe.

Msimu uliopita ilipocheza mechi 30 bila kupoteza hakukuwa na kelele nyingi pamoja kusimama dakika kadhaa kupiga makofi au wachezaji kuonekana wanacheza kwa ajili ya 'Unbeaten'. Walikuwa wakicheza kwa kuusaka ubingwa ambao walikuwa wameukosa kwa misimu minne mfululizo, na kweli wakaupata. Msimu huu walionekana kucheza ili kulinda 'Unbeaten' kitu ambacho kiliwafanya wakati mwingine kucheza kwa wasiwasi.

Baadhi ya viongozi wao kuifanya ni ajenda, kutangazwa sana kenye vyombo vya habari na kuwahimiza mashabiki kusimama kila inapofika dakika ya namba ya 'Unbeaten' ilizidi kufanya wachezaji watumie nguvu zaidi kuilinda badala ya ufundi, kiasi cha kuonekana kuchezeshwa wachezaji tegemeo ambao ni majeruhi, badala ya kuwapanga wachezaji wengine wazima. Ina maana ilikuwa inajipa yenyewe presha ya 'Unbeaten.'

Nadhani imefika wakati Yanga kuachana na hilo. Na kwa sababu tayari imeshavunjwa, wanatakiwa kuwapumzisha baadhi ya wachezaji ambao wameonekana wanafatiki. Mbali na Ligi Kuu, Yanga ikumbuke imeshatinga hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, huko kuna ushindani wake, ukichanganya na Kombe la FA msimu huu itacheza mechi nyingi sana, hivyo iwe na tahadhari na afya za wachezaji.

# Watoto 443,000 kuchanjwa polio

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WATOTO 443,230 wenye umri chini ya miaka mitano mkoani Singida wanatarajia kupatiwa chanjo dhidi ya ugonjwa wa kupooza (polio).

Mratibu wa Huduma za Chanjo Mkoa wa Singida, Habibu Mwinory, akizungumza jana wakati wa uzinduzi alisema kampeni hiyo ni ya awamu ya nne iliyoanza Disemba Mosi na itahitimishwa kesho. Uzinduzi huo ulifanyika katika Hospitali ya Sokoine iliyoko Manispaa ya Singida.

Mwinory alisema katika kuhakikisha chanjo hiyo inafanikiwa dozi 478,000 zimesambazwa katika halmashauri zote saba za mkoa wa Singida kuanzia Oktoba 31, mwaka huu.

Alisema siku ya kwanza ya kampeni hiyo, watoto 126,875 walipatiwa chanjo sawa na asilimia 114 kiwango ambacho ni zaidi ya lengo la mkoa la kutoa chanjo kwa watoto 110,807.5 kwa siku.

"Nawaomba wananchi wajitokeze kuwaleta watoto na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa watoa huduma za afya wakati wa kampeni na hatimaye mkoa wa Singida tuweze kuchanja watoto wote na kufikia lengo la mkoa," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, akizungumza katika uzinduzi huo, aliwataka wakuu wa wilaya kupitia kamati za afya za msingi za halmashauri (PHC) kusimamia utoaji wa huduma za chanjo kwenye vituo ili kuhakikisha lengo la kutoa chanjo kwa asilimia 100 linafikiwa.

Aidha, alisema wakurugenzi wa halmashauri zote na watumishi waweke mpango mkakati wa kuhakikisha watoto waliokosa chanjo mbalimbali wanapatiwa ili kuepuka kutokea kwa mlipuko wa magonjwa yote yanayozuilika kwa chanjo ukiwamo wa polio

"Wananchi mjitokeze kushiriki kampeni hii mkumbuke kwamba mtoto asiyepata chanjo ni hatari kwa maisha yake na kwa jamii inayomzunguka kwani anaweza kuambukizwa au kuwaambukiza wengine ugonjwa kwa kutokuwa na kinga," alisema.

Serukamba alisema chanjo itakayotolewa ni ile ile ambayo hutolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya na ni salama na inatolewa bila malipo na wataalam.

Aliongeza kuwa pamoja na kutekeleza kampeni ya polio awamu ya nne, kutakuwa na tendo la umezaji dawa za minyoo na kichocho kwa watoto wenye umri wa kwenda shule kuanzia miaka minne hadi 14.

Mkuu huyo wa mkoa alisema suala hilo pia litawahusu watoto wenye umri huo wasio shuleni kwenye shule zote za msingi na mkoa umeweka lengo la kumezesha



Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka (kushoto), akimnadi mgombea ubunge wa Jimbo la Amani Zanzibar kwa tiketi ya CCM, Abdul Yussuf Maalim, katika mkutano wa uzinduzi wa kampeni za CCM, jimboni humo juzi. **PICHA: FAHAD SIRAJ WA CCM**

# Shaka: CCM ndiyo yenye uwezo wa kuleta maendeleo Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimewataka wananchi katika Jimbo la Amani kumchagua mgombea iliyemsimamisha kwa kuwa ndiye mwenye uwezo wa kuendeleza kazi nzuri ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi.

CCM imesema Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, amefanya kazi kubwa na nzuri, hivyo anastahili kupewa viongozi watokanao na CCM ili kuendeleza kazi hiyo.

Hayo yalisemwa juzi na Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya uchaguzi mdogo wa Jimbo la Amani, Zanzibar na kumnadi mgombea wa CCM, Abdul Yussuf Maalim.

Alisema kazi ya kuleta maendeleo hususan katika jimbo hilo, haiwezi kuletwa na kila mtu, hivyo kuna umuhimu mkubwa wa kumchagua mgombea aliyesimamishwa na CCM.

"Kazi ya kuleta maendeleo ya nchi hii hapewi kila mtu. Kazi ya kuleta maendeleo Jimbo la Amani si kila mmoja anaweza. Wapo wenye uwezo wa kuleta propaganda kwenye jimbo la Amani, lakini wapo wenye uwezo wa kuleta maendeleo wana Amani mkasema kweli haya ni maendeleo ambayo tunayahitaji, ndiyo maana tukasema Abdul songa mbele nenda ukapeperushe bendera ya Chama Cha Mapinduzi.

"Ushindi wa CCM katika jimbo la Amani ni kama kufa na kupona.

Tutashinda kwa haki, tutashinda kwa amani lakini tutashinda tukiwa wamoja na tumeshikamana," alisema.

Shaka alisema kazi nzuri iliyofanywa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, kipindi cha miaka miwili ni kubwa, hivyo anastahili kupongezwa na kuungwa mkono ikiwamo kumchagulia wagombea watokanao na CCM.

"Ndani ya kipindi cha takriban miaka miwili ya uongozi wa Dk. Mwinyi mtu apende asipende, afurahi asifurahi, Dk. Mwinyi ameupiga mwingi (amefanya vizuri kuleta maendeleo). Mabadiliko tunayoyashuhudia Zanzibar lazima tukubali matarajio ya Wazanzibari kwa Dk. Mwinyi ni makubwa zaidi," alisema.

Akizungumza katika kampeni hizo, Abdul alisema iwapo atachaguliwa kuwa mbunge wa jimbo hilo, amejipanga kuendeleza kasi ya maendeleo kwa kushirikiana na Rais Dk. Mwinyi na viongozi wengine wa chama, serikali na wananchi kwa ujumla.

Uchaguzi huo unatarajiwa kufanyika Desemba 17, mwaka huu, kutokana na kifo cha aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Maalim Mussa.

# Mfumo kuwezesha biashara za wanawake na vijana waundwa

**Na Frank Monyo**

MFUKO wa Kuendeleza Sekta ya Fedha Tanzania (FSDT) umeziwezesha taasisi za fedha nchini kuunda muungano utakaowezesha upatikanaji wa Huduma Jumuishi za Fedha kwa Biashara Ndogo na za Kati (MSME) zinazosimamiwa na wanawake na vijana.

Akizungumzia muungano huo jana, Mkurugenzi Mkuu wa FSDT, Pamela Shao alisema uamuzi wa kuunda muungano huo ulijitokeza baada ya kongamano la MSME zinazomilikiwa na kusimamiwa na wanawake na vijana lililofanyika hivi karibuni jijini Dar es Salaam.

"Kupitia muungano huu, taasisi wanachama zitawezeshwa kifedha na kiufundi ili kuziwezesha kuimarisha uwezo wao katika utoaji wa huduma za kifedha kwa biashara ndogo na za kati.

"Taasisi wanachama pia zitapata fursa ya matangazo kupitia njia za vyombo vya habari ili kuzifikia biashara ndogo na za kati nyingi zaidi ambazo hazijafikiwa na benki," alisema.

Shao alisema kupitia hatua zinazofaa, sekta ya fedha inaweza kuchukua nafasi kubwa katika kujenga mazingira wezeshi ya ukuaji wa biashara ndogo na za kati.

Miongoni mwa washiriki waliokubali kuundwa kwa muungano huo, aliwataja kuwa ni wakurugenzi wakuu, wakuu wa idara za kuhudumia wafanyabiashara ndogo na za kati na mameneja wa benki za biashara ndogo na za kati.

Wengine aliwataka kuwa ni taasisi za huduma ndogo za kifedha kutoka Akiba Commercial Bank, Bank of Africa, ASA Microfinance Tanzania, DCB Commercial Bank, FINCA Microfinance Bank, Letshego Bank, Mwanga Hakika Commercial Bank, People's Bank of Zanzibar, United Bank for Africa, Access Bank, NCBA Tanzania, TCB Bank, Maendeleo Bank, Vision Fund Tanzania na BRAC International.

Washiriki wengine aliwataja ni wakurugenzi kutoka Creditinfo Tanzania, DOT Tanzania na maprofesa kutoka Shule ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mwanga Hakika Bank, Jagjit Singh alisema muungano huo utawawezesha kupata huduma za fedha zinazofaa ili kuwahudumia vyema wanawake na vijana wenye biashara ndogo na za kati.

Alisema kundi hilo kwa sasa linaonekana kuwa ni hatarishi kwa watoa huduma za kifedha kutokana na biashara zao kutokuwa rasmi.

# Wachungaji waonywa tamaa ya vyeo

**Na Kulwa Mzee**

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Assemblies of God Gospel Church International (AG-GCI), Dk. Asumwisye Mwaisabila amewaasa wachungaji kutenda kazi ya Mungu kwa weledi na kutaka asiwapo mtu wa kutamani vyeo.

Askofu Mwaisabila alitoa angalizo hilo jana alipozungumza na wachungaji wa kanisa hilo kuhusu kusudio la kuitisha harambee Jumapili kwa ajili ya kukusanya Sh. milioni 120 za ujenzi wa Makao Makuu ya Kanisa jijini Dodoma.

Aliwataka wachungaji wa kanisa hilo kuwaelimisha washirika wao kuhusu harambee hiyo ambayo aliitaja kuwa ni njia kuu ya ufadhili wa kanisa.

"Wachungaji tufanye kazi ya Mungu kwa weledi kama wito wetu ulivyo, asiwapo mtu mwingine wa kuinuka tofauti na wenzake kwa kutamani vyeo, ninataka kuliona kanisa hili linasimama vizuri," alisema.

Kiongozi huyo aliishukuru serikali kwa kuendelea kuisimamia amani ya nchi na kutoa uhuru wa kuabudu kwa watanzania.

Alisema wanaendelea kumwomba Mungu mvua iendelee kunyesha na kuondokana na hali ya ukame iliyokuwa inatishia usalama wa nchi.

"Ninawahasa waumini wa madhehebu tofauti kuendelea kukemea pepo la ajali nchini, ninawakumbusha madereva wachukue tahadhari wanapokuwa barabarani na wazingatie alama za barabara," Askofu Mwaisabila alisema.




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maluum, Dk. Dorothy Gwajima (kushoto), akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto Duniani, yaliyoandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa ya kuhudumia watoto (UNICEF), yaliyofanyika mkoani Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TCRS kutenga fedha elimu ya Ukimwi

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

SHIRIKA la Kikristo la Kuhudumia Wakimbizi (TCRS), linatarajia kutenga bajeti kwa ajili ya kutoa elimu kwa vijana na watoto ili kuwahamasisha kutojiingiza kwenye tabia za ngono na uhusiano kabla ya ndoa.

Hatua hiyo pia itasaidia kujikinga na maambukizi mapya ya ugonjwa wa Ukimwi yanayoonekana kuongezeka hasa kwa watoto wa chini ya umri wa miaka 15 na vijana kati ya miaka 15 na 24 wilayani Morogoro.

Ofisa Mwezeshaji wa TCRS, Gasper Lyimo, alisema hayo juzi kwenye maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika kiwilaya katika uwanja wa Soweto, Kiroka tarafa ya Mkuyuni yenye kaulimbiu isemayo 'Imarisha Usawa'.

Lyimo alisema TCRS hutoa elimu kupitia vikundi vya uhamasishaji wilayani hapa kuanzia mwaka 2006 kwa kutumia ngoma na nyimbo ambazo zinajaribu kuelimisha, kuonya na kutoa makaripio kwa masuala mbalimbali yanayohusu jamii.

Alisema licha ya kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi kwa jamii nzima, bajeti watakayoitenga itasaidia kulenga zaidi vijana na watoto, makundi ambayo yameonekana kuwa na maambukizi, hivyo kutishia nguvu kazi ya taifa.

Kwa mujibu wa Lyimo, elimu watakayoitoa itawafanya wajitambue kama ni vijana wanaopaswa kusimama na kutenda mambo mema na kuepukana na maambukizi mapya ya Ukimwi kwa sababu katika umri huo, vijana hujiingiza kwenye uhusiano bila kujua wanachokifanya.

"Tunata elimu ya kujengea uwezo kwa jamii hasa kwa watu wa hali duni kimaisha ili kubadilisha kutoka hali ya chini kwenye umaskini, kuwaimarisha kufikia ngazi nyingine ya kupata mahitaji ya msingi ya kila siku," alisema.

Alisema TCRS hufanya kazi za kuelimisha katika kata nne zilizoko wilayani Morogoro ambazo ni Mikese, Tomondo, Kiroka na Tawa kwa kuwajengea uwezo katika mambo mbalimbali yakiwamo maendeleo huku msisitizo ukiwa hakuna maendeleo kama kuna Ukimwi, hivyo wahamasike kubadilisha tabia na mienendo inayoweza kusababisha kuongezeka maambukizi yanayoleta athari kubwa za umaskini.

Lyimo alizitaja sababu kubwa zinazochangia ongezeko la maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VVU) ni maendeleo ya kidunia (utandawazi) ambayo huwafanya watoto au vijana kujihusisha na uhusiano wa kimapenzi na kushuka kwa maadili katika jamii. Pia alisema wako watu wazima wanaowashawishi watoto katika umri mdogo kuwa na uhusiano hivyo kusababisha kupata maambukizi ya VVU.

Meneja wa TCRS Mkoa wa Morogoro, Rehema Samwel, alisema awali mwaka 2021 walitenga na kutumia Dola 500 za Marekani ambazo ni sawa na Sh. milioni 1.1 katika kuwajengea uwezo wanaoishi na VVU, kusaidia watoto yatima katika masuala ya elimu ikiwamo kuwapa sare za shule na madaftari na kuwajengea uwezo vijana kupitia michezo pamoja na matamasha ya upimaji wa VVU kwa hiari.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando, alisema ni vyema elimu ikazidi kutolewa kuanzia shule za msingi juu ya Ukimwi ili kupunguza maambukizi kwa watoto chini ya miaka 15 na vijana.

Msando alisema maambukizi mapya kwa vijana wa umri wa miaka 15 na kuendelea kundi ambalo linakwenda kwenye ukuaji ni hatari kwa sababu huongezeka maambukizi kwenye makundi mengine, hivyo kurudisha nyuma nguvu za kuondoa au kupunguza maambukizi mapya ya ugonjwa huo kwenye wilaya hiyo.

# Watunukiwa tuzo umahiri kitaaluma

**Na Joseph Mwendapole**

WANAFUNZI 96 wa Chuo Kikuu Ardhi (ARU), wametunukiwa tuzo mbalimbali kutokana na kufanya vizuri kitaaluma kwa mwaka wa masomo 2021/22.

Wanafunzi hao walikabidhiwa tuzo hizo jana chuoni hapo na Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Evaristo Liwa, kwenye hafla fupi ya kuwapongeza huku wanafunzi wa kike, Happiness Sanga, akiibuka mshindi wa jumla.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo, Taaluma, Utafiti na Ushauri, Prof. John Lupala, alisema sherehe za kuwazawadia wanafunzi hao kila mwaka zimekuwa zikiwezeshwa na wadau mbalimbali.

Aliwataja baadhi ya wadau waliotoa tuzo hizo kuwa ni Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Bodi ya Wathamini Tanzania (VRB), Bodi ya Usajili wa Wabunifu na Ukadiriaji Ujenzi (AQRB), African Property Limited, Taasisi ya Wabunifu na Wakadiriaji Ujenzi (TIQS), Mekon na Webb Uronu and Partners.

Aliwapongeza wadau hao na kuwaomba waendelee kuunga mkono jitihada za wanafunzi hao kwani zawadi mbalimbali zinazotolewa na wadau hao zimekuwa zikisaidia kuongeza ari ya utendaji kazi kwa wanafunzi.

Prof. Lupala alisema tuzo hizo zimekuwa zikisaidia sana kuongeza tija kwenye maisha ya wanafunzi ya kielimu na kiuchumi huko wanakokwenda kufanya kazi.

"Kwenye sherehe za mwaka huu tuna wanafunzi 96, kati yao wasichana ni 50 na wavulana ni 46 ambao wamefuzu kupata tuzo na zawadi mbalimbali kwa vipengele mbalimbali vya kitaaluma," alisema Prof. Lupala.

Aliwapongeza wanafunzi wote waliopokea tuzo hizo na kuwataka waendelee kuweka jitihada kwenye masomo yao ili waje kuwa mfano wa kuigwa kwa wanafunzi wenzao na jamii kwa ujumla.

Prof. Liwa alisema sherehe za utoaji tuzo chuoni hapo zitafuatiwa na shughuli ya mahafali siku yatakayofanyika desemba 6, mwaka huu. Wahitimu 930 watatunukiwa shahada na stashahada zao na aliwapongeza kwa kufikia hatua hiyo muhimu kwenye maisha yao.

"Nawapongeza sana wahitimu na baadhi yao wamekuwa wakipokea tuzo mbalimbali kwa miaka kadhaa mfululizo hii inamaanisha kwamba kwenye juhudi ya kweli mafanikio hupatikana ni matumaini ya chuo kuwa juhudi hizo mtaziendeleza kwenye shughuli za ujenzi wa taifa," alisema

## Milioni 200/- zatumika miradi ya afya Arusha

**Na Allan Isack,** ARUMERU

UJENZI wa miundombinu ya afya katika kata tatu za Halmashauri ya Arusha wilayani Arumeru umekamilika baada ya serikali kutoa fedha za utekelezaji wake.

Katika mwaka wa fedha wa 2021/22, serikali ilitoa Sh. milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba nne za watumishi kwenye kata nne za halmashauri hiyo.

Lengo la kutolewa kwa fedha hizo ni kuboresha miundombinu kwenye vituo hivyo na kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi wa maeneo hayo kwa muda wote.

Akizungumza jana na waandishi wa habari mjini hapa, Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi alisema kiasi hicho cha fedha kimetumika kujenga nyumba nne za watumishi wa afya kwa gharama ya Sh. milioni 50 kwa kila nyumba.

"Fedha hizo zimejenga nyumba za watumishi kwenye maeneo ambayo watumishi hawakuwa na mahali pa kuishi kwa kuwa walilazimika kuishi mbali na vituo vyao vya kazi, nyumba hizi zimejengwa kwenye zahanati za LoovLukuny na Ilkerini, Kata ya Kisongo, Zahanati ya Ilkirevi Kata ya Oltoroto na Kituo cha Afya Nduruma," alisema Mkurugenzi Msumi.

Mkuu wa Idara ya Mipango katika Halmashauri hiyo, Anna Urio alisema fedha hizo ni utekelezaji wa malengo ya bajeti ya halmashauri ya mwaka wa fedha 2021/22 ulioishia Juni mwaka 2022 kwa kuboresha mazingira ya watumishi ili kuongeza tija na ufanisi katika kazi.

Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Ilkirevi, Kata ya Olturoto, Atu Sanga alisema kuwapo nyumba ya mtumishi wa afya kutaongeza tija na ufanisi wa kazi, ikiwamo kutoa huduma za afya kwa saa 24.

"Mtumishi akiishi eneo la kazi inampunguzia gharama za kulipa kodi ya nyumba, pia inatuwezesha kutoa huduma za dharura hasa nyakati za usiku, wagonjwa wanakuwa na uhakika wa kupata matibabu," alisema Mganga huyo Mfawaidhi.

Diwani wa Olturoto, Baraka Mollel aliipongeza seikali kwa utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika sekta zote hususani sekta ya afya, kwa kuwa sekta hiyo ni muhimu kwa afya za wananchi.

"Ninaipongeza serikali kwa niaba ya wananchi wa Olturoto, ujenzi wa nyumba ya mtumishi ni wazi utaongeza tija katika utendaji wa kazi, pia uwanda mpana wa upatikanaji na utoaji wa huduma za afya kwa wananchi sambamba na kupunguza vifo vya wanawake na watoto," Mollel alifafanua.

# Manyara na Simiyu kufunguliwa kiuchumi

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

SERIKALI imepanga kuifungua kiuchumi mikoa ya Manyara na Simiyu baada ya kuridhia kuanza kwa mradi mkubwa wa ujenzi wa barabara ya lami yenye urefu wa kilomita 63 kutoka Karatu kupitia Mbulu/Hydom hadi Maswa.

Mradi huo utakaoanza kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha, ulitangazwa jana na Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Manyara (TANROADS), Bashir Rwesingisa wakati wa kikao cha Bodi ya Barabara.

"Katika mwaka wa fedha 2022/23, serikali inakusudia kutekeleza miradi minane ya ujenzi wa barabara kwa kushirikiana na wabia wa maendeleo. Tayari Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imetangaza miradi yote hiyo itafanywa kwa kutumia mfumo mpya wa EPC Plus Finance na Mkoa wa Manyara.

"Mradi wa kwanza wa kimkakati ni ule unaohusisha kuifungua mikoa ya Manyara na Simiyu. Lakini pia uko mradi utakaojengwa kuanzia Handeni/Kiberashi mpaka kwa Mtolo mkoani Singida ukihusisha barabara yenye urefu wa kilometa 460.

"Kwa Mkoa wa Manyara, itajengwa barabra ya kilometa 120 kuanzia Karatu/Mbulu Hydom mpaka Maswa yenye urefu wa kilometa 63. Kwa ujumla Mkoa wa Manyara utajenga kilometa 505 kati ya kilometa 1,302 ambazo zinatakiwa kujengwa kwenye miradi hiyo," alibainisha.

Rwesingisa aliitaja miradi mingine itakayotekelezwa ni pamoja na Arusha/Kibaya (Wilaya ya Kiteto hadi Kongwa Mkoa wa Dodoma) ambapo Mkoa wa Manyara peke yake zitajengwa kilometa 322 za barabara ya lami.

Hivi karibuni, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, akiwa mkoani hapa, alisema kuanzia sasa serikali inaanza kutumia mfumo mpya wa kisasa wa 'EPC Plus Finance' ambao katika nchi niyingine duniani umekuwa ukirahisisha ujenzi wa barabara za kiwango cha lami kutekelezwa kwa muda mfupi.

Waziri Mbarawa alinukuliwa akisema mfumo huo utaanza kutekelezwa nchini kupitia miradi mitatu ya ujenzi wa kiwango cha lami kwa barabara za Mkoa wa Manyara zenye urefu wa kilometa 1,320.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Zanzibar Fedha na Mipango, Jamal Kassim Ali (wa tatu kushoto), akikabidhi tuzo ya mshindi wa jumla katika uandaaji na uwasilishaji bora wa taarifa za hesabu za mwaka 2021, iliyotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) kwa Mkuu wa Fedha wa kampuni ya Tanga Cement Plc, Isaac Lupokela, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. Tanga Cement pia iliibuka mshindi wa kwanza kwenye kipengele cha wazalishaji kwa mwaka wa sita mfululizo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC akabidhi kadi za bima kwa familia zenye WAVIU

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arusha, Said Mtanda amekabidhi kadi 100 za huduma ya bima ya afya kwa kaya 20 zenye watu wanaoishi na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (WAVIU), huku akiwaonya baadhi ya watu wanaoendelea kuwanyanyapaa watu hao, akisisitiza kufanya hivyo ni sawa na kutenda makosa ya ukatili.

Mbali na onyo hilo, Mtanda pia amewataka WAVIU kuzingatia ushauri wanaopewa na wataalamu wa afya na kuepuka ulevi wa kupindukia na matumizi ya dawa za kulevya ili afya zao ziendelee kuimarika kwa muda wote.

Mtanda alikabidhi kadi hizo juzi wakati wa maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani yaliyofanyika jijini hapa, akisema serikali imejipanga kikamilifu kuendelea kutoa huduma za ushauri nasaa na upatikanaji wa dawa za kupunguza makali ya ugonjwa huo bila malipo.

"Wananchi wanaoishi na watu wenye maambukizi ya virusi vya UKIMWI ni marufuku kuwanyanyapaa kwa namna yoyote, kwa sababu hawa ni Watanzania wenzetu na wana haki sawa. Tabia ya kuwanyanyapaa wagonjwa wa aina hii imepitwa na wakati. Kufanya hivyo ni ushamba. Ukijiona uko salama, usidhani kuwa wewe ni mkamilifu," alisema.

Katika hatua nyingine Mtanda alisema bado jitihada zinahitajika za kukabiliana ugonjwa huo kutokana na maambukizi ya VVU kwa Wilaya ya Arusha kuongezeka kutoka asilimia 2.8 mwaka 2020 hadi asilimia 3.1 kwa mwaka 2021.

"Bado tuna jukumu la kukabiliana na maambukizi ya VVU wakati serikali ikiendelea na jitihada za utoaji wa dawa za kupunguza makali ya virusi pamoja kuimarisha mfumo wa utoaji huduma kwa watu wenye maambukizi," alisema.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Hargeney Chitukulo alisema halmashauri hiyo itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kutoa bima za afya kwa watu wenye maambukizi ya VVU ili wapate huduma za afya muda wote.

"Leo siyo mwisho wa kutoa kadi za bima ya afya kwa wenye VVU na kaya maskini. Halmashauri tutaendelea kutenga fedha kwenye bajeti zetu ili tuendelee kutoa kwa watu wengi zaidi," alisema.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Konga cha WAVIU katika Halmashauri ya Jiji la Arusha, Caroline Chami aliviomba vyombo vya watunga sera kuwaingiza watu wenye maambukizi ya VVU kwenye mfumo wa serikali wa kupatiwa mkopo wa asilimia 19 kama yalivyo makundi mengine ili waweze kujikwamua kiuchumi.

"Tunaishukuru serikali tunapata ushirikiano wa kutosha licha ya kukabiliwa na tatizo la kunyanyapaliwa na baadhi ya watu. Tunaomba wadau mbalimbali kutoka sekta binafsi na watu wenye mapenzi mema kuendelea kuwasaidia watu wenye maambukizi ya VVU," alisema.



## Taasisi yatoa somo ulinzi wa mazingira

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

TAASISI ya kimkakati ya Siha Sports Agency imemtaka Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Seleman Jafo kuja na mwongozo maalum mahususi wa kuzisukuma Halmashauri za Wilaya hiyo kuanzisha mpango kabambe wa kuilinda miti yote inayooteshwa kwa kutumia kifaa maalum cha kukokotoa mawasiliano ya kijiografia (GPS).

Kifaa hicho kina uwezo wa kulinda uharibifu wa miti hiyo kwa kuchukua matukio yote yanayoendelea na kuyarusha kupitia mfumo wa satelaiti na teknolojia hiyo ya Global Positioning System.

Akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa kampeni ya upandaji miti katika Hospitali ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi ya Kibong'oto iliyoko Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, Mwenyekiti wa Siha Sports Agency, Selina Mkonyi alisema ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi yanayoendelea kwa sasa, ni vyema miti yote iliyooteshwa na inayoteshwa na wananchi au taasisi mbalimbali ifuatiliwe kwa kutumia kifaa hicho.

"Tumekuja kuzindua kampeni hii ya upandaji miti Kibong'oto kwa sababu Kibong'oto ni Hospitali ya Taifa inayoshughulika na Magonjwa Ambukizi hasa TB (kifua kikuu) UVIKO-19, Ebola na wagonjwa yote yanayoambukiza.

"Tunalenga kuwafanya wananchi wa taifa letu kuwa na afya, kwa kuwa miti ni uhai. alisema tunafanya uzinduzi wa Siha afya Marathon kupitia uoteshaji wa miti pia kwenda na lengo la taifa la kutokomeza ukame na kuleta uoto wa asili.

"Tunajiunga na harakati za kitaifa, tunajua kwamba wizara inayoshughulika na mazingira inalo jukumu la kuotesha miti na kuhamasisha uoteshaji miti.

"Hivi sasa taasisi nyingi zimeanza kuifuatilia kidijitali miti inayopandwa kwa kutumia GPS, sisi tunafikiri tuungane nao na watutafute na sisi tuwatafute, kwa sababu tunajenga nyumba moja," alisema.

Kuhusu uhusiano uliopo kati ya afya marathon, kifua kikuu na kifua kikuu sugu, Mkonyi alisema kifua kikuu ni ugonjwa wa mapafu na mapafu ni kiungo kikubwa cha hewa, hivyo Watanzania wakiwa na miti inayotoa hewa ya Oksijeni kwa wingi ni lazima watapata afya.

Februari 2 mwaka huu, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango alizindua Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 ambayo pamoja na mambo mengine, inaelekeza kuwa kazi ya kuhifadhi mazingira, ikiwamo kulinda vyanzo vya maji, misitu, upandaji miti, kupendezesha miji, ni lazima kuanzia sasa kuwa kazi za kudumu.

Akizindua kampeni hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu aliagiza Halmashauri ya Wilaya hiyo kushirikiana na wadau wa mazingira, wakiwamo Siha Sports Agency, kupanda miti katika maeneo yenye ukame ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi yanayotesa binadamu na mifugo kwa sasa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Dancan Urassa alisema wilaya hiyo inatishiwa na tatizo katika baadhi ya maeneo kukosa miti, hasa ukanda wa tambarare kuanzia West Kilimanjaro, Kata za Ormelili, Donyomurwa, Orkolili, Makiwaru na Karansi ambazo zinakaliwa na idadi kubwa ya jamii za kifugaji na wakulima.

# Tanga yatajwa tishio kwa watoto wanaotelekezwa

## ■ Wataka operesheni ndoa jinsia moja

**Na Oscar Assenga,** TANGA

MKOA wa Tanga unatajwa kuwa na asilimia 40 ya watoto waliotelekezwa na wazazi wao vijijini na kukimbilia mijini kutafuta riziki, huku wadau wa haki za binadamu wakionya kuwa kadhia hiyo inachochea kasi ya ongezeko la matukio ya ukatili wa kijinsia.

Jana, Ofisa Uhamasishaji wa Jamii kupitia Mradi wa Vijana Balehe dhidi ya Visa vya Ukatili, Suleiman Msey alisema jijini hapa kuwa utelekezaji huo wa watoto unaathiri familia nyingi za mkoa huo kwa sasa.

"Maeneo ya vijijini kuna visa vingi vya ukatili ambavyo vinachochewa na baadhi ya babu na bibi ambao wameachiwa kulea watoto, kutotambua sheria.

"Utafiti wetu unaonyesha wazazi na walezi kushindwa kutimiza wajibu wao wa malezi na kukimbia majukumu hayo ndicho kiini cha ongezeko la ukatili.

"Huko vijijini kuna watu tumebaini kwamba watoto wanapokwenda kuchunga mbuzi, wanajaribu na wanapoona tamu, kesho anajaribu kwa mwenzie. Jambo ambalo ni hatari kwao," alionya.

Kutokana na ongezeko hilo, Msey alimshauri Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba na Mkuu wa Wilaya, Hashim Mgandilwa, kuanzisha operesheni maalum za kuwatafuta watu wanaofanya vitendo vya ovyo ikiwamo ushoga.

Wakati wa ufunguzi wa mdahalo huo, Mkurugenzi wa Asasi ya Tanga Youth Talent Association (TAYOTA), George Bwire alisema hali ya ukatili wa kijinsia kwa Jiji la Tanga ni mbaya kwa kuwa kuna idadi kubwa ya watoto wanaofanyiwa vitendo vya ulawiti wakiwa na umri mdogo.

Alisema mdahalo huo unakwenda sambamba na kuwajengea uwezo waandishi wa habari kushiriki katika kutokomeza ukatili nchini.

Alisema kabla ya kuanza kutekeleza mradi huo, walifanya utafiti na kupata taarifa za awali kuhusu hali ya ukatili mkoani Tanga.

Alisema shirika limedai kuwa hali hairidhishi kutokana na kwamba bado watoto wafanyiwa ukatili wa hali ya juu.

Alisema watoto ambao wamekuwa wakikumbana na mikasa hiyo, wengi wao ni wenye umri wa kuanzia miaka minane mpaka 10 na wengine wanafanyiwa na ndugu zao wakiwamo baba wa kambo.



Mkuu wa Shule ya Sekondari ya kata ya Magila, wilayani Muheza, mkoani Tanga, Shehe Semtawa (kushoto), akizungumza katika mahafali ya kidato cha nne ya shule hiyo, jana. Wanafunzi 111 wamehitimu kidato cha nne. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Sera Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu yapitiwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imeanza kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Huduma na Maendeleo ya Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2004 ili kujibu mahitaji ya sasa ya wanawake wenye ulemavu.

Mapitio hayo yanafanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu baada ya kuona huduma za afya na ushirikishwaji wa wanawake ni muhimu katika kuleta maendeleo endelevu nchini.

Uamuzi huo ulitangazwa jana jijini Arusha na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi alipozindua kongamano la wanawake wenye ulemavu lililoandaliwa kwa lengo la kujadili masuala ya ujumuishwaji katika huduma za afya.

Alisema serikali imeendelea kujipambanua katika kuweka mazingira rafiki, jumuishi na wezeshi kwa makundi yote, wakiwamo wanawake wenye ulemavu.

"Miongoni mwa kazi zinazofanywa na serikali mbali na kufanya mapitio hayo ni pamoja na kuboresha huduma za afya kwa wanawake, pia kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi yao," alisema.

Naibu Waziri Katambi alisema tayari serikali imeanza kuelekeza majengo yake na vituo vipya vya afya na mengineyo yanayotoa huduma kwa umma, kuzingatia mahitaji maalum ya wanawake wenye ulemavu, wakiwamo wajawazito wenye ulemavu.

"Pili, utekelezaji wa mpango kazi wa kitaifa wa kutokomeza ukatili wa wanawake na watoto wa mwaka 2017/18 hadi 2021/22 umefikia mwisho na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Makundi Maalum, UN Women na wanawake wenye ulemavu tulikutana nao Singida kutoa maoni ya awamu ya pili ya mpango huo ili utakapokamilika na kuzinduliwa uwe na sura maalum yenye vipaumbele vya wanawake na watoto wenye ulemavu," alisema.

Baada ya kauli hiyo ya serikali, Mratibu wa Mradi wa Wanawake, Uongozi na Haki za Kiuchumi, Erasmina Massawe aliipongeza serikali kwa kuweka kipaumbele katika mahitaji ya watu wenye ulemavu, akisema dhamira kubwa inayoonyeshwa inatoa taswira kwamba haki za wenye ulemavu zinalindwa, sauti zao zinasikika na wanaishi maisha ya heshima, utu na yenye fursa sawa.

"Takwimu zinaonyesha kuwa zaidi ya watu bilioni moja duniani wanakabiliwa na aina fulani ya ulemavu, ambapo wastani wa asilimia 19.2 ni wanawake wenye umri wa miaka 18 kulinganisha na wanaume asilimia 12 ambao wanakabiliwa na ulemavu," alisema.

Kwa Tanzania alisema idadi ya watu wenye ulemavu inakadiriwa kuwa ni zaidi ya milioni 2.225 na kati yao asilimia 57.3 ni wanawake na asilimia 42.7 ni wanaume.



## Wahitimu waandaliwa mazingira ya kujiajiri

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKURUGENZI wa Mipango wa Wizara ya Fedha na Mipango, Moses Dulle amesema serikali imetengeza mazingira yake kwa ajili ya wahitimu wa vyuo ili wajiajiri.

Dulle alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na wanachuo wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini Dodoma kwa ajili ya kuwakutanisha na wanataaluma ili kubadilishana uzoefu.

Alisema tayari serikali imeshaandaa mazingira yake ya kuhakikisha wanachuo wanaohitimu waungane kwa pamoja na kuandika maandiko ya kuomba fedha ili kujiajiri.

"Sisi kama serikali tunawaomba wanaohitimu kwenye chuo cha mipango wajikusanye kwa pamoja ili waandike andiko litakalowawezesha kutengeneza mazingira ya wao wenyewe kujiajiri," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema serikali itaendelea kuimarisha vyuo vyake vya mipango ikiwamo miundombinu yake ili wanafunzi wapate elimu iliyoboreshwa na kuwawezesha kupata ajira.

Alisema vyuo vya mipango vipo kwa ajili ya wanafunzi kupata maarifa na ujuzi utakaowawezesha kumudu maisha yao ya kila siku.

"Ni imani yangu wanaosoma kwenye vyuo vya mipango walio wengi wanapata ujuzi na maarifa namna ya kujiinua kiuchaumi wao wenyewe na jamii kwenye maisha ya kila siku," alisema.

**Alisema vyuo vya mipango vipo kwa ajili ya wanafunzi kupata maarifa na ujuzi utakaowawezesha kumudu maisha yao ya kila siku.**

# Usimamizi mzuri Ushirika wapunguza malalamiko

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

USIMAMIZI mzuri wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania umepunguza malalamiko ya wakulima wanaouza mazao yao kwa mfumo wa stakabadhi ghalani.

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Laurean Ndumbaro aliyasema hayo jana alipozindua Baraza la Wafanyakazi wa Tume hiyo jijini hapa.

Alisema usimamizi huo umesaidia wakulima kupokea fedha za malipo yao kwa wakati na kuondoa malalamiko yaliyokuwa yakijitokeza.

"Ninapongeza Menejimenti ya Tume hii kwa ufanyaji kazi wao wa kufuata kanuni na miongozo ya kiutumishi, Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume pamoja na menejimenti yake wamekuwa wakifanya kazi nzuri ya kuwahudumia wananchi walio katika Ushirika kupata haki na stahiki zao kwa wakati.

"Mnafanya mambo mazuri, malalamiko yamepungua kwa wakulima wanaouza mazao yao kwa stakabadhi za ghalani maana wanapokea fedha za malipo yao kwa wakati, huu ndiyo utumishi unaohitajika katika serikali yetu," alisema.

Aliwakumbusha watumishi wa tume kuzingatia uadilifu, uwajibikaji, bidii na ubunifu pamoja na haki kwa kuwa ndiyo nguzo kubwa kwenye utumishi wa umma.

Dk. Ndumbaro pia aliitaka tume hiyo kuhakikisha wakulima wanaacha kuuza mazao yao yakiwa shambani.

"Mpango wa kuanzisha Saccos ndani ya Amcos utamlinda mkulima na kumsaidia kupata fedha pale wanapokuwa na uhitaji, hivi mnafikiri wakulima wetu wanapenda kuuza mazao yao kwa bei rahisi kabla ya kuyatoa shambani? Hapana! Ni shida ndiyo zinawafikisha hapo walipo, sasa wasaidieni waache tabia za kuuza maua au mazao kabla ya kuvuna," alisema.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa tume hiyo, Dk. Benson Ndiege alimwomba Katibu Mkuu kuipa kipaumbele na kuitazama tume kwa jicho la kipekee kama taasisi ya kimkakati ili kufanikisha ufumbuzi wa matatizo yanayowakabili.

Dk. Ndiege alisema vyama vimechangia ongezeko la pato la taifa na kwa mwaka 2019/20 hadi 2021/ 22, tani milioni 9.8 za mazao ya kimkakati ziliuzwa kupitia vyama na Sh. trilioni 2.9 zililipwa kwa wakulima na serikali imepata tozo za kodi mbalimbali kupitia mamlaka zake.

Pia alisema kuna ongezeko la viwanda vidogo, kati na vikubwa 279 vilivyoanzishwa chini ya mfumo wa uendeshaji wa vyama vya ushirika.




Wafanyabiashara wakiendelea shughuli zao, katika soko jipya la kisasa la Machinga, jijini Dodoma, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# 'Maofisa biashara simameni katika taaluma kufikia lengo'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji imewataka maofisa biashara nchini kusimamia taaluma zao ili kufikia lengo la kuwa mfano bora wa uwezeshaji wa biashara kwenye mamlaka za serikali za mitaa.

Jijini hapa jana, Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Biashara katika wizara hiyo, Christopher Mramba alitoa kauli hiyo alipozungumza kwa niaba ya Waziri, Dk. Ashatu Kijaji kwenye uzinduzi wa Chama cha Maofisa Biashara Wanawake (TAWTO).

Mramba alisema katika utekelezaji wa majukumu yao, maofisa biashara wanapaswa kuhakikisha wanakuwa wawekezaji wa biashara na si wakwamishaji.

Aliwataka kutoa elimu na kuwasaidia wafanyabiashara kutambua wanachopaswa kufanya ili kukuza na kuboresha biashara zao.

Alisema katika kutekeleza lengo kuu la kuwezesha biashara, wanawatumia maofisa biashara wanawake kutoka taasisi kwa kushirikiana na maofisa biashara waliopo chini ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwenye halmashauri zote nchini ili kutengeneza mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara wadogo na wakubwa.

Awali akiwasilisha taarifa ya chama hicho, Mwenyekiti wake, Elizabeth Swagi alisema licha ya kuwapo juhudi kadhaa kwa upande wa serikali na sekta binafsi katika kuwasaidia wanawake wafanyabiashara, bado wanakumbana na vikwazo mbalimbali hasa katika sekta isiyo rasmi.

Alitaja vikwazo hivyo ni pamoja na kiwango kidogo cha elimu kuhusu biashara, taratibu ndefu au urasimu katika kuanzisha biashara kutokuwa na mtaji wa kutosha, kukosekana kwa mikopo yenye riba nafuu, kunyimwa haki ya kumiliki mali, hivyo kukosa dhamana ya mikopo.

"Suala lingine ni sheria na kanuni kulenga zaidi kampuni kubwa na kusahau wafanyabiashara wadogo na wa kati na unyanyasaji wa kijinsia, ikiwamo ukatili wa kingono unaofanywa na baadhi ya maofisa kwenye sekta ya biashara," alisema.

Aliomba wizara kuwaruhusu na kuwawezesha wanachama wao kushiriki mikutano mbalimbali inayoandaliwa na chama na kuchangia gharama za uendeshaji wa mikutano hiyo.

Katibu wa chama hicho, Bertha George alisema wameamua kuwa na chama hicho kwa wakati huu kutokana na utandawazi ili kuendana na mapinduzi ya sayansi na teknolojia.





# Taasisi ya kusimamia uwajibikaji yazinduliwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi, amezindua taasisi mpya ya Ofisi ya Rais ya Utekelezaji na Usimamizi wa Shughuli za Serikali (PDB) ambayo itakuwa na lengo la kuongeza kasi ya utekelezaji na usimamizi wa ahadi zake kwa wananchi.

Akizungumza katika hafla hiyo iliyofanyika jana katika viwanja vya Ikulu, Zanzibar, Dk Mwinyi alisema taasisi hiyo itaanza na sekta nne ambazo ni miundombinu, utalii, uchumi wa bluu na huduma za kijamii ili kuwa na mfumo utakaoruhusu kuzingatia rasilimali na umakini katika usimamizi na kupata matokeo ya haraka.

Alisema kupata mafanikio kunahitaji kuwapo vipaumbele na shabaha zinazoweza kupimika na mipango makini pamoja na ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kutatua matatizo yanayojitokeza.

Dk. Mwinyi alisema tayari kuna wafanyakazi wa awali wa taasisi hiyo kuanza kazi ya kusimamia utekelezaji wa shughuli za serikali kwa maono watakayoelekezwa.

"Jukumu kubwa la msingi wa taasisi hii ni kuhakikisha utekelezaji wa vipaumbele nilivyovitaja kwa wakati unaofaa" alisema Dk Mwinyi.

Aidha alisema lengo la taasisi hiyo ni kusaidia kusukuma utekelezaji na si kubadilisha majukumu ya wizara bali kumsaidia kusukuma mambo yaende kwa haraka zaidi.

Taasisi hiyo, alisema itasaidia kuondoa vikwazo, kubaini uhaba wa rasilimali na masuala mengine ambayo yanaweza kuchelewesha maendeleo ya nchi.

"Katika kufikia lengo la kujenga Zanzibar ya ndoto zetu, ni dhahiri kuwa hatuwezi kuendelea kutumia utaratibu wa zamani katika ulimwengu mpya. Lazima tubadilishe na kuharakisha njia zetu za kufanya kazi. Tunapaswa kuacha kufuata njia za kawaida na kufanya kazi mambo kwa mazoea. Lazima tuwe makini na tuonyeshe utekelezaji," alisema.

Dk Mwinyi alisema lazima utumishi wa umma uboreshwe ili kutoa huduma bora kwa wananchi na kuwa na miundombinu imara, utalii endelevu, uchumi wa bluu na maendeleo ya kijamii yaliyo shirikishi na endelevu.

Rais alisema kipimo cha mafanikio ni kuongeza ajira, kutoa huduma bora katika elimu, afya, maji na sekta zingine za kijamii ili kupunguza umaskini na kuboresha maisha ya wananchi kama walivyoahidiwa.

Alisema ni dhamira ya serikali yake anayoiongoza kuyafikia matarajio hayo ya wananchi na kutoa wito kwa wananchi kushirikiana kwa vitendo na taasisi hiyo iliyozinduliwa ili kutoa matokeo madhubuti.

Mwakilishi wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Christine Musisi, aliipongeza serikali ya Zanzibar kwa kuanzisha taasisi hiyo ambayo itasaidia katika kufikia lengo la kutoa huduma kwa wananchi kwa mwendo kasi na ufanisi wa hali ya juu.

Alisema UNDP inaamini kwamba PDB itakuwa daraja kubwa linalounganisha fursa mbalimbali na mahitaji ya serikali, sekta binafsi na wananchi kwa ujumla.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akisaini kitabu cha maombolezo kufuatia kifo cha Rais mstaafu wa Jamhuri ya Watu wa China, Jiang Zemin, katika ubalozi wa Mdogo wa China, Mazizini, jijini Zanzibar jana. Kushoto ni Balozi Mdogo wa China, Zhang Zhisheng. **PICHA: IKULU**

# Urari wa biashara wapanda bil. 61.1/-

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Divisheni ya Takwimu za Utoaji wa Huduma, Bakari Khamis Kondo, amesema Oktoba, mwaka huu, urari wa biashara umeongezeka na Sh. bilioni 61.1 zimepatikana.

Akizungumza jana na waandishi wa habari mjini Zanzibar, alisema uwiano wa usafirishaji na uagizaji umeongezeka kutoka asilimia 24.8 kwa Septemba, mwaka huu, hadi asilimia 28.7 kwa Oktoba.

Bakari alisema bidhaa zilizosafirishwa Oktoba zilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 24 .6 ambalo ni ongezeko la asilimia 33.7 ikilinganishwa na Oktoba, mwaka jana.

Mkuu huyo alisema kundi la vyakula na nyama linaongezeka kwa kuchangia asilimia 96.8 ya thamani yote ya usafirishaji wa bidhaa Zanzibar.

Alisema usafirishaji wa bidhaa kwa nchi tano zilizoongoza kwa Oktoba, mwaka huu, umefikia asilimia 96.1 ya thamani ya bidhaa zote zilizosafirishwa huku Indonesia ikiwa imeongoza kwa bidhaa zenye thamani ya Sh. milioni 19,537.8 sawa na asilimia 79.3 ikifuatiwa na Singapore, China, Kenya na Vietnam.

Pia alisema bidhaa zilizoagizwa Oktoba, zina thamani ya Sh. bilioni 85.7 huku thamani ya bidhaa zilizoagizwa imeongezeka kwa asilimia 0.6.

Mkuu huyo alisema thamani ya bidhaa za walaji imepungua kwa asilimia 10.7 ikilinganishwa na Oktoba, mwaka jana na kwa asilimia 7.8 ikilinganishwa na Septemba, mwaka huu.

Mtaalamu wa masuala ya uchumi kutoka Benki Kuu ya Tanzania, Dk. Ulrick Mumburi, alisema benki hiyo imejipanga kuhakikisha fedha za kigeni zinapatikana wakati wote ili wanunuzi na wanaoagiza bidhaa wapate mahitaji ya fedha za kigeni.

Alisema kwa vile Zanzibar imeonekana iko vizuri katika kununua na kuuza bidhaa katika mataifa mbalimbali, wajibu wao kwa sasa ni kuendelea kutoa usharikiano ili uchumi kukua zaidi .

# Zanzibar yaweka mikakati kupambana na Ukimwi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar imesema imejipanga kupambana na ugonjwa wa Ukimwi ikiwamo maambukizi mapya dhidi ya vijana na kuepukana na matukio ya kuwanyanyapaa wagonjwa.

Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, alisema hayo juzi katika maadhimisho ya kilele cha Siku ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika katika Uwanja wa Jadida, Pemba.

Othman alisema utafiti uliofanywa umebaini kuwapo kwa kasi ya maambukizi ya ugonjwa huo kwa kundi la vijana huku yakiwamo matukio ya maambukizi ya makusudi.

Alisema serikali inaendelea na mikakati yake kuhakikisha watu wote walioambukizwa virusi vya Ukimwi (VVU) wanajitambua ili kuacha tabia ya kuambukiza wengine kwa makusudi.

Pia alisema baada ya kundi hilo kufahamika wanatakiwa kuhakikisha wanatumia dawa kwa ajili ya kupunguza maumivu yanayotokana na maradhi nyemelezi. Alisema lengo ni kuona kwamba vitendo vya udhalilishaji vya kuwanyanyapaa watu wanaoishi na VVU vinaondoka moja kwa moja ili kuwawezesha kuishi kwa furaha.

"Hiyo ndiyo mikakati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kukabiliana na kupambana na ugonjwa wa Ukimwi. Tunataka kuona matukio ya udhalilishaji na kuwanyanyapaa wenye VVU yanaondoka moja kwa moja," alisema. Aidha, aliitaka Tume ya Kudhibiti Ukimwi, kufanya tathmini ya kina kuhusu maendeleo ya ugonjwa huo ili kuhakikisha ifikapo mwaka 2030 maambukizi yanapungua kwa kiasi kikubwa.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Said Suleiman, alisema Tume ya Kudhibiti Ukimwi itaendelea na majukumu yake ya kutoa elimu kwa jamii juu ya athari za ugonjwa huo kwa taifa hasa kwa vijana ambao ndio nguvu kazi ya taifa.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk Khatib, aliwataka wananchi kupima afya zao mara kwa mara zaidi wale ambao hufanya safari za nje yakiwamo makundi ya wavuvi.



## WOLPER

UKURASA 16

Nipashe
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI DESEMBA 3, 2022



# MAPENZI TU

UKURASA WA 18

YUKO WAPI ?

# FREDDIE NDALA KASHEBA-3

# Mchawi wa gita 'kombora', akalivunja na kuzikwa nalo



**Na Adam Fungamwango**

WIKI iliyopita tulimtazama mwanamuziki Freddie Ndala Kasheba akiwa na bendi yake ya Orchestra Fauvette wakiwa wamerejea nchini Zaire (sasa Congo DR) na kubadilisha jina la bendi kutoka jina la zamani na kujiita Safari Nkoy ikiwa na maana ya 'Chui Msafiri', wakarejea tena nchini na kurekodi vibao kama 'Fula Matamba', 'Zinzele', 'Luka Yayo', 'Sina Ndugu' na Mijumbe ya Kasongo'.

Nyimbo mbili za 'Sina Ndugu' na "Mijumbe ya Kasongo' zilitungwa na King Kiki ambazo alikuja tena kuzirudia akiwa na Maquis du Zaire katikati ya miaka ya 1970, akaziita 'Nasema Sina Ndugu' na 'Kasongo Rudi Kijijini'.

Kwa mara nyingine tena, bendi hiyo ilirejea nchini Zaire mara tu baada ya kutoka kurekodi nyimbo zao nchini Kenya.

**Arejeshwa nchini na King Kiki**

Nilichogundua ni kwamba huwezi kuelezea historia ya Kasheba bila ya kumtaja King Kiki. Kwani baada ya kuwa wote kwenye bendi ya Fauvette iliyobadilishwa jina baadaye ikaitwa Safari Nkoy, wakaja kuwa pamoja mwanzoni mwishoni mwa miaka ya 1970 na mwanzoni mwa 1980 wakiwa na bendi ya Orchestra Safari Sound (OSS) ikiyokuwa ikitumia mtindo wa 'Masantula Ngoma ya Mpwita'.

Wengi hawajui hili. Wanachofahamu ni kwamba mwanamuziki huyo alikuwa kiongozi wa OSS wakati wa mtindo wa 'Dukuduku'.

Ukweli ni kwamba Kiki na Kasheba walikuwa wote kwenye OSS ya Masantula ya mwanzo kabisa, kama walivyokuwa kwenye Fauvette.

Hata hivyo, aliondoka baadaye na kwenda kufanya shughuli za muziki nchini Burundi.

Ilikuwaje? Baada ya Safari Nkoy kurudi Zaire, Kiki alikutana na wanamuziki wa bendi ya Maquis du Zaire Lubumbashi, akawadithia juu ya biashara ya muziki nchini Tanzania inavyolipa, na akawashawishi kuja.

Hii ndiyo sababu ya Maquis kuja nchini katikati ya miaka ya 1970, na miaka michache tu baadaye Kiki naye alirejea nchini na kujiunga na bendi hiyo.



Mwishoni mwa miaka hiyo, 1979, alichukuliwa na mfanyabiashara Hugho Kisima kwenda kuongeza nguvu kwenye bendi ambayo haikuwa maarufu, OSS iliyotumia mtindo wa 'Nyekese Paradise', na alipotimba tu, akaibuka na mtindo wa 'Masantula Ngoma ya Mpwita' uliojipatia umaarufu mkubwa.

Lakini  alimwita rafiki yake Kasheba kutoka Zaire wakawa wote kwenye bendi hiyo.

Hata hivyo kabla hawajarekodi wimbo wowote, Kasheba akaondoka kwenda nchini Burundi.

OSS ilivuma kama moto nyikani kutokana na vibao vyake vikali kama 'Ni kweli', 'Mtoto wa Mjini', 'Haruna Kaka', Mwaka wa Watoto' na vingine vingi.

Miaka michache baadaye mkataba wa Kiki na bendi hiyo ulimalizika kwa namna ya kushangaza hakuongezwa, badala yake akarudishwa nchini Kasheba na kukabidhiwa bendi hiyo.

Kiki akarejea tena kwenye bendi yake ya zamani ya Maquiz, huku Kasheba akiuondoa mtindo wa Masantula na kuutambulisha wa kwanza aliouita 'Dukuduku'.

**Itaendelea**

## UDAKU TU

# Majigambo ya Ray Kigosi, yamliwaze Steven Kanumba



MKONGWE wa filamu za Bongo Muvi, Ray Kigosi maarufu kama Ray, wiki hii ameibuka na kutangaza kurejea ulingoni baada ya ukimya wa muda mrefu.

Ray ametamba kurudi na ari mpya iliyojaa mabadiliko ya filamu na kuonyesha umwamba wake wa siku nyingi.

Jina la Ray na marehemu Steve Kanumba, yalikuwa yakitamba katika tasnia ya filamu kiasi ambacho kiliwafanya mashabiki kushindwa kugawanyika linapokuja suala la nani mkali kati yao.

Hata hivyo, wakati akizungumza na wanahabari mwigizaji huyo amesema anarudi akiwa mkamilifu kutokana kwamba anajiamini kuwa yeye pekee anaweza kuja na mabadiliko ambayo wengi wanayahitaji.

Ametaja mambo yanayokwamisha tasnia ya filamu isisonge mbele kuwa ni ufinyu wa bajeti, wasanii kutumia muda mfupi na uchache wa vipaji vipya.

"Mimi ni mkubwa katika nchi hii, huwezi kuitaja filamu bila kunitaja mimi, nimerudi tena nikiwa na nguvu mpya ya kuleta mabadiliko na hatimaye kurudisha uhai wa filamu nchini,"

Daudi Chiwane, amesema ukubwa wa Ray utakuja pale tu atakapofanikiwa kuinua tena sanaa ya filamu ambayo kimsingi imenza kufufuka kwa kusuasua.

Amesema kujigamba kwamba yeye ni mtambo wa kutengeneza wasanii, hakutoshi kama hakutaonekana jitihada binafsi ambazo zitaleta vipaji vipya na kuongeza thamani ya kazi kama ilivyokuwa zamani.

"Watu wamezoea kusikia majigambo, majivuno na simulizi mbalimbali za kuinua tasnia ya filamu, lakini hakuna kilichopatika, tunataka kumuona Ray akiyafuata haya na kuonyesha anaweza," amesema.

Aidha, amesema kuwateta nchini wasanii kutoka Ghana, Nigeria na hata Marekani ni jambo zuri, lakini isipoangaliwa kwa umakini inaweza kuleta athari kwa waigizaji wa hapa nchini.

"Mwenyewe amekiri kwamba hakuna vipaji vipya kwa sasa baada ya Wolper, Uwoya na Wema, naamini kama hakutaangaliwa vya kutosha kuwachukua waigizaji wa nje kutadumaza vipaji vya hapa nchini," ameongeza kusema.

Amemshauri msanii huyo kufanya utafiti wa kutosha wakati anapoingia rasmi katika fani ili lengo lake la kuurudisha umaarufu wa filamu za Bongo ufanikiwe, pengine anaweza kumliwaza mshindani wake Kanumba ambaye kifo chake kimechangia kuporomosha sanaa hiyo.

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**





**@shamsaford**
Kuna muda mwingine Mungu anakuepusha na mabalaa kwa kukukosesha vitu unavyopigania kuwa navyo karibu.

**@richmitindo**
Usije kuacha duka wazi ukakimbiza mwizi, Ni sawa ulichokiona kwa mchepuko kuna mtu kakiona kwa mkeo, kama uelewa wako mdogo usirudie kusoma.






**@Elizabethmichaelofficial**
Bwana Elon mwisho utuuwe kwa slesi, haya tuanzage kufanya mazoezi..! na bei za fotoshuti zitapanda. TUMEPATIKANA

**@roma_zimbabwe**
Vandame aliwapiga watu wengi saaana, wengine miamba haswaaa, na hakuwahi kupigwa kwa muda mrefu.
Siku moja alikutana na bwana mdogo tu, tulizoea kumuita #BrandonLee
DAME ALIPIGWA KAMA NGOMA!!



**BASI SAWA**

## Furaha Sophie afunga mwaka



Kutoka nchini Australia, mwimbaji maarufu wa gospo Furaha Sophie, amewataka mashabiki wa muziki huo kukaa tayari kwa ujio wa ngoma yake mpya, kwa imani.

Akizungumza na BT, Furaha amesema huo ni mwendelezo wake wa kujisogeza kwa mashabiki wa Afrika Mashariki ndio maana amekuwa akiachia nyimbo mbalimbali ndani ya mwaka 2022.

"Mwaka huu nimefanikiwa kuachia nyimbo kubwa kadhaa ambazo zimefanya vizuri, nafunga mwaka na audio na video mpya ya wimbo Kwa Imani, naamini utapokewa vizuri na mashabiki zangu hapo Afrika Mashariki," amesema Furaha.

## Staa wa 'Squid Game' kortini



STAA wa filamu iliyopendwa zaidi duniani, 'Squid Game', O Yeong-su amefunguliwa mashtaka ya unyanyasaji wa kingono.

Mwendesha mashtaka wa Korea Kusini amesema kuwa, O Yeong-su mwenye umri wa miaka 78, anatuhumiwa kwa kumgusa isivyofaa mwanamke mmoja mwaka 2017.

O Yeong-su mwezi Januari alitangazwa kama Mkorea Kusini wa kwanza kutwaa tuzo ya Golden Globe.



# WOLPER ASIMULIA MAGUMU YA HARUSI

MWIGIZAJI mkongwe wa Bongo Muvi, Jacqline Wolper, amesema harusi yao wametumia kiasi kisichopungua milioni 200, lakini hawajaishiwa kifedha.

Amesema katika harusi yao na mume wake Rich Mitindo, ambayo ilifana sana imemfundisha mambo mengi ikiwamo kuwapata marafiki wapya na kuwajua vizuri wale wa zamani.

"Kuna mambo mengi yamejifunza kwenye harusi yangu, lakini yote namuachia Mungu kwa sababu nimepata marafiki wapya na kuwajua vyema wale wa zamani. Nashukuru tumemaliza salama na kizuri hatujaachwa bila fedha kutokana na wengi wamenichangia," amesema.



# Obby ataja mafanikio 2022

MWIMBAJI wa nyimbo za Injili, Obby Alpha amesema mwaka 2022 kwake umekuwa mzuri baada ya kupata mafanikio katika kazi zake.

Obby Alpha amesema kwake umekuwa mwanzo mzuri baada ya kuandaa kazi zaidi ya 10 ambazo wakati wowote ataanza kuziachia moja moja.

"Mwaka 2022 umekuwa wa mafanikio kutokana na kufanya kazi katika mazingira rafiki zaidi, kuwa na video 10 tena zimeongozwa na waongozaji wakubwa hapa Tanzania sio kazi rahisi," amesema Obby Alpha.

## NOVEMBA IMEMALIZWA KIBABE

**Na Adam Fungamwango**

TUKO kwenye mwezi wa mwisho wa mwaka 2022, ambapo kila mtu anaangalia kile alichokipanda na kukivuna kwa mwaka mzima.

Wasanii, waigizaji na wanamuziki wanaangalia ni nini walichokifanya kwa mashabiki wao, kuwatolea filamu bora na ngoma za uhakika, huku wao wenyewe wakijiangalia kimewaingizia nini.

Tunaangalia mwezi Novemba ambao kuna wasanii waliamua iwe iwavyo hauwezi kupita bila kutoa ngoma.

Nazileta kwenu ngoma zote kali zilizobamba kibabe mwezi Novemba.

**Jux ft Zuchu-Nidhibiti**

Tarehe kamili ya kutoka kwa ngoma hii haijajulikana. Lakini inaonekana ilianza kusikika kwenye mitandao ya kijamii kuanzia Novemba 20 hivi. Na mpaka sasa bado ngoma hiyo 'Nidhibiti' ipo kwenye audio, bado haijafanyiwa video, lakini imeanza kuteka mashabiki wa muziki wa bongo fleva. Ni msanii Jux akimshirikisha Zuchu.

"Kama mapenzi kitabu, ungekuwa ukurasa wa katikati, ukichanwa wewe stori haiendelei." Ni baadhi ya maneno yaliyo kwenye ngoma hiyo.

**Aslay vs Harmonize-Follow Me**

Msanii Aslay amerejea. Mwezi Novemba umemrudisha msanii huyu mwenye sauti nyororo. Katoa ngoma yake aliyoiita 'Follow Me.' Ngoma hiyo iliyo kwenye video imetolewa Novemba 29, akimshirikisha mmoja wa wasanii wakubwa nchini Harmonize. "Unakula nyama hadi mifupa, unataka nini nitakupa." Anaimba Aslay kwenye wimbo huo wa mapenzi.

**Barnaba ft Nandy-Tamu**

Mwezi Novemba mambo ni moto. Hapa Jux na Zuchu, halafu huku kuna Barnaba na Nandy. Hawa walianza kutoa ngoma Novemba 12 waliyoiita 'Tamu' Ngoma ni ya Barnaba ambaye anaeleweka kwa umahiri wa utunzi wa mashairi, halafu akaona amshirikishe Nandy. Barnaba anasema penzi lake ni la udi, kumpenda hana budi. Hata video yake ni kali, Nandy anamletea Barnaba maua.

**Ali Kiba-Asali**

Mkongwe Ali Kiba naye hakuwa nyuma mwezi huo. Tarehe 29 naye alifyatua ngoma yake akaiita 'Asali', nayo imeshaanza kuteka mashabiki kwenye mtandao wake wa instagram.

Ameimba kisawasawa kama kawaida yake. Si unajua Kiba huwa hana 'mbambamba?'

**Marioo-My Life**

Sijui niseme nini, hii ni Novemba tu, Desemba itakuwaje? Watu watamalizaje mwaka? Si watauana? Tarehe 29 Marioo naye aliona isiwe tabu akatoa ngoma yake 'My Life' Hapa ukiangalia, ngoma zote nne zimetoka siku moja.

Hii inaonyesha kuwa watu hawana mchezo, sasa tusubiri ngoma za kumalizia mwaka 2022.



**FILAMU**

# Montana: Penzi kizungumkuti

**Na Adam Fungamwango**

MSONDO Ngoma Music Band iliwahi kutunga wimbo waliouita 'Penzi Kizungumkuti.' Kwenye wimbo huo wanalielezea penzi kuwa ni jambo ambalo halieleweki vema. Ni kizungumkuti kitupu. "Wala usishangae kuona mtaani kwenu kuna sherehe, wawili wapendanao wanafunga ndoa, pale mtaa wa pili kuna kijana amejinyonga kwa sababu ya mapenzi, ama mapenzi ni kizungumkuti, yanaweza kuua wakati wowote." Ni baadhi ya mashairi yaliyomo kwenye wimbo huo.

Ni wimbo unaoelezea ukweli kuhusu mapenzi. Ni kama umeme. Ukitumiwa majumbani unakuwa rafiki kwani utawasha taa, utaangalia televisheni na kila kitu ambacho kinahusika. Lakini ukipata shoti unaweza kupata hasara ya kuunguza vitu wakati mwingine hata nyumba.

Tuliangalie penzi kwenye filamu ya 'Montana ambayo imetungwa na Ibrahim Kitimbu, ikachezwa na Kudra Mshengeli, Shizoh Manizoh, Zainabu Omari aliyecheza kama Montana na Salma Ally.

Montana ni msichana mrembo mno, akiishi kwenye eneo fulani mtaa fulani. Aliwavutia wanaume wengi. Mshengeli na Shizoh walikuwa ni moja ya wanaume waliotokea kumtamkia kuwa wanampenda.

Awali mwenyewe hakujua nani amkubali na nani amkatae. Ghafla tu penzi likaangukia kwa Mshengeli. Lakini hakumwambia Shizoh ambaye naye aliambiwa asubiri atajibiwa. Shizoh akawa na matumaini kibao.

Katika hali isiyotarajiwa kumbe Shizoh na Mshengeli ni marafiki wakubwa. Montana akawa amewagonganisha wanaume wawili bila kujua. Marafiki hao wakikutana kila mmoja anamsimulia mwenzake juu ya kumiliki msichana mrembo. Kila mmoja alikuwa akitoa sifa ya msichana wake, bila kujua ndiyo huyo huyo mmoja.

Hata hivyo moyo wa Montana uliangukia kwa Mshengeli. Sasa Shizon akaanza kudanganywa tu, akipewa matumaini ambayo hayapo.

Siku isiyo na jina, Shizoh alikutana laivu na Mshengeli akiwa na Montana. Msichana huyo na Shizoh walipatwa na mshituko, huku Mshengeli akiwa hajui nini kinaendelea. Hakujua kuwa Montana na Shizoh wanafahamiana.

Mshengeli akamfahamisha rafiki yake kuwa aliyenaye ndiye mpenzi wake ambaye kila siku huwa anamhadithia habari zake.

Shizoh hakusema lolote, na wala hakuonekana kama amefadhaika. Alipomaliza kusalimiana na kutambulishwa na rafiki yake, hakuonekana kufanya jambo lolote ambalo lingemfanya Mshengeli ajue lolote kuhusu mpenzi aliye naye.



Hata hivyo aliondoka na lake moyoni. Alitaka kujiua kama si kaka yake kumuwahi. Kama mtu alimtafuta Montana na kumwambia juu ya yote yaliyojitokeza. Akamkanya kutocheza na hisia za watu.

Wakati Shizoh akitoka hospitali, Montana akaambiwa ahame eneo lile aende mbali na mpenzi wake kwa sababu iwapo Shizoh siku akimuona, au akiona wapo pamoja na mpenzi wake Mshengeli anaweza kufa kwa presha.

BONGO FLEVA

# NI MAPENZI TU



SIRI iliyomfanya mwanamuziki maarufu wa Bongo Fleva, Barnaba kubadili dini imeelezwa ni mapenzi yaliyopitiliza kwa mke wake mtarajiwa Raya Sykes.

Mwimbaji huyo mashuhuri, amebadili dini na sasa anaitwa Mohamed badala ya lile la awali la Barnaba.

Akizungumza katika sherehe ya kuvishana pete, mama Kimbo ambaye ni mama mkwe wa Barnaba, amesema suala la kubadili dini hakulazimishwa kama moja ya masharti ya kumchumbia binti yao, bali yeye mwenyewe binafsi aliamua.

"Hatukumlazimisha kubadili dini, ila yeye mwenyewe aliamua na sasa anaitwa Mohamed Elias, hata mwanangu angeamua hilo tusingempinga tungemuacha huru kwa sababu dini zote zinaamini Mungu mmoja," amesema Mama Kimbo.

Amesema hata jina hilo kachagua mwenyewe kwa utashi wake, hivyo anaamini wamechukua maamuzi hayo kutokana na kupendana kwa dhati.

Barnaba alimvisha pete ya uchumba mpenzi wake huyo wa muda mrefu siku ya Jumatatu katika hafla ndogo.

Katika picha ambazo walichapisha kwenye kurasa zao, wachumba hao wawili walivalia nguo nyeupe wakati wa tukio hilo muhimu katika mahusiano yao.

Raya amesema kuwa Barnaba humfanya ajisikie ameheshimika kwa kumchumbia na ameahidi kumpenda maisha yote.

Aidha, alidokeza kuwa huenda ndoa yao ikafungwa siku si nyingi kuanzia sasa.

"Umejua kuniheshimisha mume wangu mtarajiwa! Naahidi kukupenda leo mpaka mwisho wa maisha yangu Barnaba," amesema Raya.

# BATA LA WIKI

Je una kiwanja cha burudani piga -0717336368

**FM Academia 'Wana Ngwasuma'**

Kila siku ya Jumamosi kama leo kundi zima la wana Ngwasuma chini ya Patcho Mwamba, hufanya vitu vyao katika ukumbi wa Mawasiliano Park Ubungo, uliopo kando ya Barabara ya Sam Nujoma, jijini Dar es Salaam.

**Tukuyu Sound Band**

Kila Jumapili vijana wa bendi hii huwa wanamalizia wikiendi yao katika ukumbi wao wa nyumbani wa Mawasiliano Park, uliopo Ubungo kando ya Barabara ya Sam Nujoma

**Orchestra Sikinde Original**

Bendi hii mpya leo Jumamosi inafanya vitu vyake katika ukumbi wa Shabaha Mbezi Becah, kesho Jumapili kama kawaida itakuwa katika ukumbi wa Nefaland Manzese Argentina.

**Waluguru Original**

Kama kawaida, bendi hii ya mjini Morogoro, kila Jumamosi hufanya vitu vyake katika ukumbi wa Terminal Pub Msamvu na Jumapili itakuwa ndani ya ukumbi wa ukumbi wa F2 Florida mjini humo.

**Town Classic Band**

Jana walikuwa ndani ya ukumbi wa Andrews (zamani T-Garden) Sinza, Leo waatakinukisha katika ukumbi wa Buga Lounge Kimara Korogwe, Jumapili wapo ukumbi ya Kibozone Malamba Mawili Mbezi.

**Kimokimo Band**

Wakiwa chini ya mwimbaji wa siku nyingi aliyepitia bendi mbalimbali, Khadija Kimobitel, kila Ijumaa huwa ndani ya ukumbi wa Mariot uliopo eneo Extertanal jijini Dar es Salaam.

**Mjengoni Classic Band**

Bendi hii ya jijini Arusha, leo Jumamosi ifanya makamuzi yake katika ukumbi wa Kokoriko Annex, kesho Jumapili itamalizia wikiendi katika ukumbi wake wa nyumbani wa Mjengoni Club Orasiti jijini humo.

**Maina Band**

Bendi hii inayoongozwa na mwimbaji mkongwe, Liston Maina, leo Jumamosi itafanya makamuzi ya nguvu katika ukumbi wa Regancy Park, Mikocheni.

**Twanga Pepeta**

Kila Ijumaa huwa wanatoa burudani ndani ya ukumbi wa Mawasiliano Park Ubungo, kesho Jummpili watamalizia wikiendi katika wa Gwambina Lounge, zamani TCC Club C hang'ombe.



# FAIDA KUZAA KITAJIRI

MWANAMITINDO Kim Kardashian, anatarajia kuvuna mamilioni ya pesa kila mwezi kama gharama ya kuwatunza watoto aliowapata na rapa Kanye West.

Kiasi hicho cha pesa kinaweza kumyumbisha Kanye, kutokana na hali ya kipato chake kudorora baada ya kampuni kadhaa alizokuwa akifanya nazo kazi kujiondoa.

Hata hivyo, mahakama moja nchini Marekani imeagiza Kim kupewa Dola 200,000 ambazo ni zaidi ya Shilingi milioni 400 kila mwezi kwa ajili ya huduma za watoto wanne.

Agizo hilo limetolewa baada ya mahakama hiyo kumaliza suala la talaka kwa wawili hao.

Kardashian aliomba talaka mwaka 2021, baada ya miaka minane ya ndoa na msanii huyo, ambaye amebadilisha jina lake kihalali na kuwa Ye.

Kuhusu mgawanyo wa mali na malezi ya watoto wao yalitatuliwa na hati za mahakama zilizowasilishwa hivi karibuni.

Pande hizo mbili zinapaswa kushauriana juu ya maamuzi kuhusu ustawi wa watoto wao, kulingana na hati hiyo ilivyosema.

Ilielezwa kwamba gharama za usalama wa watoto, shule na chuo watashirikiana kwa mujibu wa hati hizo.

Wanandoa hao wana watoto wanne: North, 9, Saint, 6, Chicago, 4, na Zaburi, 3.

Katika taarifa kadhaa zilizowasilishwa hapo awali, Kardashian (42) alisema anataka ndoa hiyo ivunjwe, akiongeza kwamba itamsaidia Kanye kuamini kwamba uhusiano huo umefikia mwisho.

Rapa huyo alizua shutuma nyingi mapema mwaka huu baada ya kuhudhuria Wiki ya Mitindo ya Paris akiwa amevalia fulana yenye kauli mbiu ya "White Lives Matter" msemo unaopingana na upingaji ubaguzi wa watu weusi.

Mapema wiki hii, Ye alitangaza nia yake ya kugombea urais wa Marekani mwaka 2024.

Awali aligombea mnamo 2020, lakini alipata kura 70,000 pekee.

## YRN atamani Takeoff angerudi



MDOGO wake rapa wa Marekani, Takeoff, ambaye alifariki hivi karibuni kwa kupigwa risasi, amesema kifo cha kaka yake kimemwacha katika mazingira magumu.

YRN Lingo, ameandika barua ya wazi kupitia mitandao ya kijamii, akisema mambo mengi hayatasalia sawa baada ya kaka yake kuuawa nje ya uchochoro wa mji wa Houston mnamo Novemba 1, 2022.

"Sikuzote ulihakikisha kuwa familia iko sawa, hata wakati sikuhitaji chochote ulinipa kitu kila wakati. Nachukia kuendelea na maisha yangu bila wewe kimwili hapa, natamani nisimamishe muda na kusubiri, lakini najua hilo haliwezi kutokea.," ameandika.



## Onyo la Tems linawahusu

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Temilade Openiyi, anayejulikana zaidi kama Tems, ametoa onyo kali kwa mtu yeyote anayejaribu kulazimisha imani zake za kidini kuathiri muziki, uvaaji na utendaji kazi wake.

Hatua hiyo inakuja baada ya mwimbaji huyo kutokea katika jarida maarufu la Dazed kukosolewa kuhusu mavazi yake yanayoelezewa hayakufuata maadili.

Kupitia ukurasa wake wa Twitter, msanii huyo alijibu maoni hayo kwa kusema kuwa yeye sio mwokozi wa mtu yeyote, na kuongeza kuwa anakataa kuingia katika muundo wowote wa kidini au maadili ili kumfurahisha mtu yeyote.

## Rita kweli una mambo wewe!

MWIGIZAJI wa Nollywood Rita Dominic, amesimulia jinsi gauni lake la harusi lilivyotaka kuharibu sherehe baada ya kuzuiwa kukosa viza ya kuingia Falme za Kiarabu (UAE) siku chache kabla ya harusi.

Rita alifunga ndoa na Fidelis Anosike wiki iliyopita mjini Yorkshire, nchini Uingereza.

Kupitia chapisho lake kupitia Instagram, amemwagia shukrani zake, mbunifu wake, Michael Nardi, ambaye alihakikisha gauni hilo linamfikia na harusi hiyo inafanyika kama ilivyopangwa.





## Will Smith anakumbuka ya Oscar

MSANII wa filamu za Hollywood na mwanamuziki, Will Smith, ameonyesha wasiwasi kuhusu ujio wa kazi yake mpya 'Emancipation', akisema bado ana kumbukumbu mbaya ya usiku wa Oscar.

Akihojiwa katika kipindi cha Trevor Noah cha "The Daily Show", mwigizaji huyo maarufu amesema ana matumaini kwamba ugomvi kati yake na Chris Rock hautaathiri mapokezi ya filamu hiyo mpya.


"Natumaini kazi itaheshimiwa na haitachafuliwa kulingana na uamuzi wa kutisha kwa upande wangu. Watu wa timu hii wamefanya kazi nzuri zaidi katika maisha yao yote. na matumaini yangu makubwa ni kwamba matendo yangu hayaiadhibu timu yangu," amesema Smith.

## Davido, Chioma wavishana pete

MKALI wa muziki kutoka Nigeria, Davido hatimaye ameamua kumvisha pete ya uchumba mpenzi wake Chioma, siku chache baada ya kumpoteza mtoto wa kiume.

Wawili hao wameonekana kuzidi kuimarisha penzi lao kwa kiwango cha juu kwa kuamua kuvishana pete kwa siri.

Walionekana kwa mara ya kwanza tangu kifo cha mtoto wao kwenye sherehe ya kuapishwa kwa Ademola wiki iliyopita, huku kila mmoja akiwa amevaa pete mkononi na kuonyesha kuwa tayari wamechumbiana.



MAKALA

# Vifaranga vya nje vinavyoua soko la wawekezaji wa ndani

**Na Mwandishi Wetu**



KATI ya sekta ambazo zinaweza kuiingizia serikali mapato ya uhakika ni pamoja na sekta ya mifugo, kutokana na kwamba ni kitowewo kinacholiwa na watu wengi kuanzia vijijini hadi mjini.

Mapato hayo yanaweza kuwa kwa njia ya uwekezaji kwenye uzalishaji wa vifaranga nchini, na kwamba wawekezaji wa ndani ya nchi wanaweza kuzalisha vifaranga na kuuza kwa wafugaji wa kuku ambao nao wanakuwa na jukumu la kukuza vifaranga na vikikuwa vinauzwa kama kuku kwa ajili ya chakula.

Licha ya uhalisia huo sekta hiyo inakabiliwa na wakati mgumu kutokana na soko kufurika vifaranga kutoka nje ya nchi, hali inayowafanya wazalishaji wa ndani kushindwa kushindana kwa sababu ya bei na gharama za uwekezaji walizonazo.

Katika kulinda soko la ndani wazalishaji, wafugaji na wauzaji wa vifaranga wa kuku wa nyama wameiomba serikali kusitisha uingizaji wa vifaranga hivyo kutoka nje ya nchi.

**HALI IKOJE**

Ufuatiliaji wa gazeti hili umebaini kuwa kuna tatizo katika udhibiti wa magendo ya uingizwaji wa vifaranga nchini ambapo vifaranga kutoka nchi za Uganda na Malawi vimekuwa vikiingia kimagendo.

Vifaranga kutoka nje ya nchi vikiingizwa hapa nchini vinauzwa kwa bei ya chini zaidi na hivyo kwa wazalishaji na wauzaji wa ndani wanajikuta wakikosa soko la kuuza vifaranga vyao, hatua inayopelekea wengine kuishia kubakia navyo ndani.

Kabla ya kukithiri kwa uingizwaji wa vifaranga kwa njia za magendo mfanyabiashara wa kati wa vifaranga anayenunua kwa wazalishaji wa ndani alikuwa anauza boksi 50 zenye vifaranga 5,000 vya kuku, lakini kwa sasa hatua hiyo imekuwa ngumu kufikiwa na kujikuta akiuza boksi tano kwa mwezi hatua inayomrudisha nyuma kimaisha.

Mfanyabiashara ya kuku wa Kimara, Haruna Hamza anaililia serikali kuanza kuchukua hatua dhidi ya uingizwaji wa vifaranga kimagendo huku akiitaka kuweka msisitizo katika kauli aliyotoa ya kusitisha vibali vya kuingiza vifaranga nchini.

Anasema licha ya uingizwaji wa vifaranga kwa njia za magendo lakini bado wizara ya mifugo imetoa vibali kwa kampuni kadhaa kuingiza vifaranga ambapo waingizaji hao wanachangia kuua soko la ndani.

"Rais Samia Suluhu Hassan anayo nia ya dhati ya kulinda soko la ndani ya uzalishaji wa vifaranga ambapo na siye tunanunua kwa wazalishaji kisha kuuza kwa wafugaji mitaani, sasa kama wakiendelea kuwepo wanaoingiza kutoka nje ya nchi na kuuza kwa bei ndogo kwa wafugaji hao hao, ni wazi kuwa siyo tunaonunua kwa wazalishaji wa ndani wote siye na wazalishaji wenyewe biashara zinaenda kufa,"anasema na kuongeza:

"Nilikuwa nafuga na kuuza kuku 3,600 kwa mwezi, ila kwa sasa hata 1,000 hawafiki na mtaji unaendelea kukata kwa hapa naona kunahitajika mjadala wa kina kwa kweli kati ya wazalishaji wa ndani na serikali."

Salima Msangi mkazi wa Gongo la Mboto anasema "Juzi nimeuza kuku mmoja kwa Sh.4,000 ni hasara sana, wakiendelea kukaa ni hasara ni bora niuze kwa hasara, soko limejaa vifaranga na kuku wengi sana, hii haina afya kwa uchumi wetu ni lazima serikali iliangalie kwa jicho la pekee."

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji wa Kuku wa Nyama Tanzania (TABROFA), Aloyce Makoye anasema kama hakutakuwa na hatua za haraka za kusaidia wawekezaji wa ndani dhidi ya vifaranga kutoka nje ya nchi, biashara ya ndani inaenda kufa.

"Mbali na kuingizwa kwa vifaranga kutoka nje kuathiri soko la ndani lakini bado kuna wingi wa kuku wa nyama wanaoingizwa sokoni kutoka nje sasa matokeo yake wazalishaji wa vifaranga wa ndani wanapata shida huku hata kwenye soko wauzaji wa kuku nao wakikumbana na changamoto," anasema Makoye.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti huyo, hali hii tete haijawahi kutokea katika biashara ya kuku wa nyama kwa kampuni zote kulalamika biashara ni nguvu.

"Ukienda Interchick, Kibo, Organia, Alvin na wengine wanalalamika biashara ni ngumu, hivyo nashauri mipaka iangaliwe, kwani tunapoenda ni pabaya na vibali vya kuingiza vifaranga kutoka nje visitolewe, ili hizi kampuni za ndani ziwe na uhakika wa soko na hivyo zizalishe kwa wingi hatua itakayowanufaisha wauzaji vifaranga wadogo wa ndani."

Mkurugenzi wa Kampuni ya Kuzalisha Vifaranga ya Organia, Albert Momdjian anasema kampuni hiyo ikiwa kama kati ya wazalishaji wa ndani pamoja na mawakala wao wanauuza vifaranga vyao wameathiriwa kwa kiasi kikubwa na uingizwaji wa vifaranga kutoka nje.

Anasema kwa sasa kampuni hiyo inaingia hasara katika undeshwaji wa shughuli zake hapa nchini kwa kuwa wanunuzi wamepungua kutokana na wengi wao kununua vifaranga vikiwemo vinavyoingizwa kimagendo kutoka nje ya nchi.

"Wadau wa uwekezaj wa biashara ya vifaranga hasa tunaozalisha hapa nchini tuliambiwa kuwa hakuna vibali vipya vinavyotolewa kwa kampuni za kuingiza vifaranga na kuwa kampuni zilizopewa vibali vyao vinatakiwa hadi sasa view vimeshaisha muda wake wa kazi," anasema Momdjian.

**KAULI YA SERIKALI**

Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo ambaye pia ni Mtoa Vibali vya kuingiza mifugo ikiwemo vifaranga, Prof. Hezron Nonga wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, anasema serikali haijatoa vibali vipya vya uingizaji vifaranga nchini na kuwataka wanaojua njia za panya waijulishe serikali.

Anasema hadi sasa kampuni zinazoingiza vifaranga ni mbili ambazo ni Wolowolo Animal Care Center na The One Agro Enterprise ambazo zilipata vibali kuanzia mwaka jana na kwamba vifaranga vinavyoingizwa ni katika kumalizia maombi yao ya zamani.

"Hizi kampuni ziliomba vibali katika kipindi ambacho nchi ilikuwa na changamoto ya uhaba wa vifaranga ambapo The One Agro Enterprise imeruhusiwa kuingiza vifaranga 494,000 kutoka Uganda na Wolowolo vifaranga 150,000 kutoka Malawi na mwisho wakuingiza ni Januari 15,2023," alisema.



# Matumizi ya dawa yanapohatarisha mwanaume kufurahia tendo la ndoa

**Na Mwandishi Wetu**

TATIZO la kupungukiwa kwa nguvu za kiume linazidi kuongezeka na kuwaathiri wanaume wengi hasa vijana ambao wanategemewa katika suala zima la uzazi.

Kutokana na tatizo hili kuwa kubwa kumekuwepo na matumizi ya kasi ya dawa za kuongeza nguvu za kiume kwa vijana wa miaka 20 hadi 35, jambo ambalo linatia hofu.

Hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan, alitaka kufanyika kwa utafiti kujua kwa nini vijana wengi wanakabiliwa na tatizo la nguvu za kiume na kujikuta wakikimbilia kutumia tiba mbadala ambazo zingine zina hatari kwa maisha yao.

Wapo wanaosema tatizo hilo linatokana na mitindo ya maisha hasa kula vyakula visivyofaa kiafya. Lakini wengine wanaeleza watoto wengi wa kiume wanaanza mapema tendo la ndoa na kusababisha nguvu za kiume kupungua.

Lakini maoni ya Rais Samia yana nguvu kisayansi, kwani bila kufanyika utafiti wa kina kujua mzizi wa tatizo hilo si rahisi kugundua chanzo, na badala yake watu wataendelea kulia tu, huku tatizo likizidi kukua kwa kasi.

Hata hivyo, kulingana na tafiti mbalimbali zilizofanyika na kuripotiwa na Shirika la Habari la Uingereza (BBC), zimegundua matumizi ya baadhi dawa ambazo zimekuwa kawaida katika familia zina athari katika nguvu za kiume.

Dawa hizo ambazo hutumiwa mara kwa mara zinapaswa kuepukwa ili vijana wasipoteze nguvu za kiume na kushindwa kushiriki kikamilifu tendo la ndoa.

Maisha yenye kukidhi matamanio ya kimwili ni moja ya mahitaji muhimu kwa binadamu, inapokosekana huwa changamoto kubwa.

Kwa mujibu wa Shirika la habari la ANI, kuna aina sita ya dawa ambazo kimsingi zinapotumiwa mara kwa mara husababisha kupunguza nguvu za kiume.

**DAWA ZA MAUMIVU**

Katika familia nyingi matumizi ya dawa za kutuliza maumivi limekuwa jambo la kawaida.Watu wengi hawasiti kutumia dawa hizo pale wanapohisi mwili una maumivu hata kama sio ya ugonjwa.

Lakini, una ufahamu kwamba dawa hizo zinaathiri uanaume wako na kuufanya usiwe na matokeo mazuri?

Kulingana na utafiti umebaini kuwa dawa za kutuliza maumivu huzuia kuundwa kwa seli za uzazi na huvuruga homoni nyingi ambazo ni muhimu katika kufanya tendo la ndoa kati ya wanaume na wanawake.



**Wapo wanaosema tatizo hilo linatokana na mitindo ya maisha hasa kula vyakula visivyofaa kiafya. Lakini wengine wanaeleza watoto wengi wa kiume wanaanza mapema tendo la ndoa na kusababisha nguvu za kiume kupungua.**



Kimsingi matumizi yaliyokithiri ya dawa za kupunguza maumivu huleta matokeo hasi baada ya kuwepo kwa mparaganyiko huo wa seli na homoni.

**DAWA ZA ANTI-ANXIETY**

Watu wengi wanaolalamika kuwa na matatizo ya akili na kuwa na wasiwasi hutumia dawa ya aina hii ili kukabiliana na hofu.

Hata hivyo, dawa kama hizo zikitumika kwa wingi hupunguza hamu ya tendo la ndoa.

Dawa hizi zinaweza kusababisha mtu kupoteza hamu ya kufanya mapenzi.

Wakati mwingine hata husababisha wanaume kupoteza hisia zao kabisa.

**DAWA YA KUGANDA DAMU**

Dawa zinazotumika kutibu kolesto, ambayo husababisha mgando wa damu, pia zina mchango mkubwa katika kupunguza nguvu za kiume.

Wataalamu wa matibabu wanasema kuwa dawa hizi huingilia utendaji kazi wa seli za uzazi.

Utafiti huo umebaini ilipotengenezwa ilikuwa itibu tatizo la moyo, lakini kwa bahati mbaya ikageuka na kuathiri nguvu za kiume.

Katika utafiti huo unaonyesha kuwa dawa zinazotumika kutibu kuganda damu wakati mwingine husababisha matatizo kwa wanaume wanapotaka kufanya tendo la ndoa na wenza wao.

**DAWA ZA SONONA**

Dawa hizi, zinazojulikana kama benzodiazepines, mara nyingi hutumiwa kutibu magonjwa ya wasiwasi, kama vile wakati mtu anaogopa vitu ambavyo havipo na yuko peke yake.

Magonjwa mengine ambayo hutumia dawa hizi ni pamoja na kukosa usingizi na maumivu ya misuli.

Lakini, upande wa madhara ni kwamba huathiri utendaji kazi wa seli za uzazi kwa wanaume na kupunguza hisia.

**DAWA ZA MOYO**

Wagonjwa wanaotumia dawa za shinikizo la damu wanaweza pia kukumbana na changamoto nyingine ambayo ni kupungua kwa nguvu za kiume.

Dawa hizi zinaingiliana moja kwa moja na mishipa ya damu na pia hufanya kazi na mfumo wa neva.

Wataalamu wengine wameongeza kuwa yapo hata matatizo ambayo wanawake pia wanakumbana nayo zinahusiana na njia za uzazi.

**DAWA ZA KIFUA**

Dawa zinazopatikana dukani kama vile dawa za kupuliza katika pua zilizoziba na dawa za kwaida za kupunguza kuziba kwa pua zina athari pia klwa wanaume.

Kulingana na tafiti imeonyesha zinaweza kusababisha matatizo katika tendo la ndoa kwa wanaume na wanawake.

Zungumza na daktari

Zungumza na daktari kama ukiona dawa unayotumia ina athari mbaya kwenye utendaji wako wa tendo la ndoa. Unasisitiziwa usiache kutumia dawa yoyote bila kuonana na daktari na kumweleza unachokiona wakati unatumia.

# Rais Ramaphosa anapokabiliwa mtihani wa kujinasua kujiuzulu

## • Bil 9.3 alizozificha shambani zamponza

Na Mwandishi Wetu




Shamba la Rais Ramaphosa linalojulikana kama Phala Phala.PICHA: BLOOMBERG

UCHUNGUZI wa kutoka kwa jopo la wataalamu wa sheria uliofanywa dhidi ya Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, umefichua shilingi bilioni 9.3 zilifichwa katika shamba lake.

Ripoti hiyo ilibaini uwepo wa fedha hizo taslimu zilizokuwa aina ya dola za Marekani milioni 4 ambazo zilihifadhiwa, kabla ya kuibiwa na wafanyakazi wake.

Hata hivyo kitita hicho cha pesa kulihifadhiwa katika shamba lake miaka miwili iliyopita umezua maswali mengi kuhusu uadilifu wa kiongozi huyo.

Jopo hilo linaloongozwa na aliyekuwa mwanasheria mkuu wa serikali, liliezea baadhi ya maelezo yaliyotolewa awali kuwa hayakuwa na ukweli.

Ripoti inayotokana na uchunguzi huo imesababisha wakosoaji wake kumtaka Rais Ramaphosa kujiuzulu na kisha kukabiliana na kesi mbele ya bunge na kwa raia wa nchi hiyo.

Kwa kuzingatia misimamo mikali ya vyama vya upinzani ambavyo baadhi yao vinamtaka aachie ngazi mara moja, kashfa hii ina uwezo wa kumgharimu nafasi yake katika taifa hilo lenye uchumi wa juu barani Afrika.

Katika wasilisho la ripoti hiyo yenye kurasa 138, ilimfanya Rais Ramaphosa kujitokeza na kukanusha kuwa hakukuwa na jambo baya kuhusu pesa hizo zilizofichwa kwenye shamba lake la kibinafsi liloko Kaskazini mashariki mwa nchi hiyo.

Ameeleza pesa hizo zilitokana na mapato ya nyati waliouzwa kwa dola 580,000 taslimu kwa raia wa Sudan, Mustafa Mohamed Ibrahim Hazim, mwishoni mwa 2019.

Hata hivyo,Hazim hajajitokeza hadharani na kwamba mtu huyo hana taarifa zozote zinazomtambulisha.

Kulingana na ripoto hiyo, ilihoji kwa nini stakhabadhi iliyowasilishwa haikuwa na maelezo yoyote ambayo yangemfanya mtu huyo atambulike.

Kulikuwa na jina lake pekee, hakuna anwani ya biashara wala nambari ya kitambulisho chake.

Hata hivyo, Rais Ramaphosa anasema mashtaka yote aliyotakiwa kuyajibu hayana msingi wowote na kwamba madai mengi yalikuwa uvumi.

Utetezi wake huo haujamuondolea shinikizo la kutakiwa kujiuzulu au ashtakiwe bungeni.

Ripoti hiyo imemchafulia sifa yake, kiongozi huyo ambaye taswira yake ya kisiasa na kupanda madarakani hadi kuwa rais kulijengwa kutokana na vita vyake dhidi ya ufisadi ndani ya chama tawala cha African National Congress (ANC).

### UCHAGUZI WA MAPEMA

Nini kitafanyika endapo Ramaphosa atathibitika na Bunge kuwa ni kweli anahusika na kashfa hiyo ambayo imebatizwa jina la "Farmgate".

Chama chake cha ANC tayari kinajadili kwa ukali na wanaeleza anapaswa kushughulikia ripoti hiyo, kulingana na vyanzo ndani ya chama vimeiambia BBC.

Wakati wengine wanamtaka kusubiri, wengine kutoka kundi pinzani ndani ya ANC, wanamtaka aondoke madarakani ili kuzuia uharibifu zaidi kwa chama.

Ofisi ya rais imesema itaishughulikia ripoti hiyo mara tu atakapomaliza kuisoma.

Rais Ramaphosa alifurahia kutokana na mapokezi mazuri kutoka ndani ya serikali, umma, wafanyabiashara na baadhi ya vyombo vya habari.

Alitoa ahadi kubwa za mapambazuko mapya kwa Afrika Kusini chini ya uongozi wake na kuwasihi wananchi waamini kwamba anaweza kubadilisha mambo, na kwamba siku za kashfa za ufisadi zingekuwa historia.

Upinzani mkuu nchini humo unasema kulingana na ripoti hiyo, rais ameonekana kuwa na kesi ya kujibu.

Chama cha Democratic Alliance kilitangaza kitatumia kikao cha bunge wiki ijayo kuwasilisha hoja ya kutaka uchaguzi wa mapema.

Kinasema shutma dhidi ya Ramaphosa zinaonyesha kwamba ANC lazima iondolewe mamlakani.

"Ripoti iko wazi na haina utata. Rais Ramaphosa kuna uwezekano mkubwa alikiuka vifungu kadhaa vya Katiba na ana kesi ya kujibu.Taratibu za kumfungulia mashtaka ni lazima ziendelee, na atalazimika kutoa maelezo ya kina kuliko alivyojielezea kwa sasa," chama kilisema katika taarifa yake.

### MASWALI MAGUMU

Ripoti hiyo iliyoundwa na hadidu rejea tatu, inazua maswali kuhusu uwasilishaji wa maandishi wa Ramaphosa wakati wa uchunguzi.

Baadhi ya hoja zilizotakiwa kupatiwa majibu ni kwa nini rais alihifadhi dola 580,000 ndani ya sofa? Kwa nini wizi wa fedha hizo haukuripotiwa polisi miaka miwili iliyopita? Na kwa nini nyati anaosema waliuzwa wanaonekana bado wako shambani kwake?

Katika maelezo ya Rais Ramaphosa, meneja wa nyumba ya kulala wageni katika shamba hilo kwanza alihifadhi pesa hizo kwenye sefu, lakini baadaye akazihamishia kwenye sofa katika chumba cha kulala cha ziada

"Ndani ya makazi yangu ya kibinafsi, kwa sababu alidhani kuwa ni mahali salama zaidi, kwani aliamini hakuna mtu angevunja na kuingia katika nyumba ya rais." Alieleza Ramaphosa wakati akijibu maswali hayo.

Hata hivyo, jopo hilo linaamini maelezo hayo yanahitaji kuchunguzwa zaidi.

Hata hivyo, upeo wa majaji ulikuwa mdogo wa kupendekeza na hivyo bunge linatakiwa kuchukua hatua.

Iwapo wabunge wataamua kwamba kamati ya kumuondoa rais ichunguze zaidi na kumpata na hatia ya utovu wa nidhamu, hilo linaanzisha mchakato wa kura ya kumuondoa madarakani.

Hatimaye itafanyika zoezi la upigaji kura ya kukosa imani, hatua hiyo inahitaji kura ya theluthi mbili bungeni ili kupitishwa.

Wakati ANC ina idadi ya kuzuia hilo kutokea, chama pia kimegawanyika.

Wanaompinga wanaweza kuona hiyo ni fursa ya kumuondoa kwa kupiga kura kutoka kwa vyama vya upinzani.



### SIFA MBAYA

Vituo vya redio vya ndani na mitandao ya kijamii vimejaa maoni tofauti kutoka kwa raia wa Afrika Kusini.

Baadhi wanaamini analengwa na maadui zake wa kisiasa, huku wengine wakionyesha kusikitishwa na kutaka aondoke.

"Hii ni mbaya sana kwa ANC," mchambuzi wa kisiasa Oscar Van Heerden aliiambia Newzroom Afrika.

Mkanganyiko huu unaweka msimamo wa maadili wa Ramphosa katika maswali.

Kibaya zaidi inaonyesha matumizi mabaya ya madaraka na pengine kukiuka katiba aliyosaidia kuitayarisha mwanzoni mwa miaka ya 1990.

Matukio haya yanajiri kabla ya kufanyika kwa kongamano la ANC mwezi huu. Ramaphosa ambaye alionekana anaweza kuchaguliwa tena kuwa kiongozi wa chama, yamemweka mwanasiasa huyo mkongwe na mkulima katika hali mbaya.

**Chanzo. BBC**

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Unakumbuka staili ya kuweka shati la shule viboksi?

- Unatia na rangi ya bluu ili uonekane nadhifu
- Unarembesha na mhuri wa shule

Na Adam Fungamwango

WADAU leo wamenitaka kuweka mada inayohusiana na staili za mavazi waliyokuwa wanavaa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wakati huo na vituko vyao.

Wala hatuendi mbali sana, ni miaka ya 1980 tu ambapo kwanza kabisa wanafunzi walikuwa na utoto na vituko vingi.

Nakumbuka ni wakati ambao baadhi ya wanafunzi ambao wazazi wao walikuwa hawana uwezo wa kuwanunulia ufutio walijiongeza, wakawa wanakata ndala au kandambili vizuri tu kwa staili ile ile. Na ilikuwa ikifuta maandishi yaliyoandikwa na kalamu aina ya penseli.

Shuleni kulikuwa na utoto mwingine wa kuunguzana na tunda za ubuyu. Mwanafunzi keshakula ubuyu wake, tunda zake anazisugua sehemu yoyote ngumu hasa kwenye sakafu, halafu anamfuata anayetaka kumuunguza. Anachofanya ni kugusisha tunda hilo na mwili wake, popote pale, lakini kwa sababu inakuwa ni michezo tu, wengi walipenda kuwasusisha mkononi au mguuni tu. Inaunguza ile mbaya. Na kama ulikuwa huna habari umekaa tu, utaruka kweli kweli.

Walimu nao walikuwa na tabia ya kuwanyoa kwa mkasi wanafunzi ambao nywele zao chafu, hawajachana nywele, au wenye nywele ndefu sana.

Staili waliyokuwa wanatumia kumnyoa denti ilimlazimu akitoka hapo na kurudi nyumbani ni lazima akamtafute kinyozi ammalizie.

Unanyolewa kama alama ya mara au msalaba. Ina maana sehemu ambazo kuna alama hiyo hakuna nywele iliyobaki. Mwanafunzi anakuwa na muonekano wa kuchukiza na kuchekesha kwa wakati mmoja.

Atataniwa na wenzake lakini hana cha kufanya kwa sababu aliyefanya hivyo ni mwalimu. Anachosubiri ni muda ufike wa kuondoka nyumbani akanyoe.

Mbali na hilo kulikuwa na staili moja kabambe ya kuweka unadhifu kwenye shati la shule. Hii ninayoitaja hapa ni mwanzoni mwa miaka ya 1980 hadi mwishoni.

Ilikuja staili ya viboksi kwenye shati la shule ambavyo muonekano wake ni kama tiara au vishada, watoto wa miaka ile wanavifahamu.

Mistari hiyo kama inavyoonekana kwenye picha ya makala hii, inakaa nyuma ya shati na hata uwekaji wake ulikuwa ni wa ufundi wa hali ya juu, na si kila mtu aliweza kuweka.



**"Hapo umemaliza, shati lilikuwa likifuliwa lazime litiwe bluu, sijui kama haya mambo bado yapo, dah. Mimi ndiyo nilikuwa nawapiga wasiojua, nilikula sana vipesa vyao kwa staili hii,**

Wanafunzi wengi walisaidiwa na kaka zao, au wakubwa zao jirani na baadhi ya madobi ambao walikuwa wanaweza kufanya utundu huo.

Mwanafunzi akifanikiwa kuweka viboksi hivyo kwenye shati basi anaonekana ni nadhifu na wenzake wote watakuwa wanamtazama.

Yeye sasa, atataka kila mmoja amuone na mikogo mingi. Atajiita 'bitozi' mwanafunzi, na mbwembwe zikizidi anaweza hata akasimamisha kola la shati.

Baadaye wengine tena wakaleta ubunifu mwingine wa kuweka rangi ya bluu kwenye shati la shule kwa ajili ya kuliongezea unadhifu.

Na kweli shati jeupe ambalo liliwekwa rangi ya bluu kwa mbali lilimfanya mwanafunzi aonekane amependeza sana kwa sababu linakuwa si jeupe sana na pia ile rangi ya bluu nayo haijitokezi kwa asilimia zote.

Ili kuipata rangi hii ilikuwa inanunuliwa na kufuliwa pamoja na shati husika. Na iliwapendeza zaidi wanafunzi wa kike kuliko wa kiume.

Halafu wanaovaa mashati hayo wawe wamevaa kaptula au sketi ya vitambaa laini ya bluu iliyokolea sana, walikuwa wanapendeza mno. Hakuna ambaye alikuwa hapendi kupendeza, lakini tatizo wakati huo ilikuwa ni uwezo.

Waliokuwa wanavaa hivyo ni wanafunzi ambao wazazi wao walikuwa na uwezo na si mwenzangu na mimi.

Kwa hali ya kawaida, wanafunzi wengi walikuwa wakinunuliwa shati jeupe na kaptura au sketi ya bluu ambazo vitambaa vyake vilikuwa kama vya khaki hivi kasoro rangi tu.

Zile sketi na kaptura zenye vitambaa laini za bluu iliyokoza bei yake ilikuwa kubwa mno na hata vitambaa vyake ukitaka kununua kumshoneshea mtoto kwa wakati huo ujipange.

Kama kawaida wachangiaji wametoa maoni yao kwenye ujumbe wa simu mitandao ya kijamii kuhusiana na mada hii.

"Viboksi hivyo tulikuwa tukivitengeneza kwa kuviweka kwenye shati kwa pasi ya mkaa, baada ya hapo kitu ng'aring'ari," aliandika mdau mmoja.

Mwingine akadai yeye alikuwa mtaalamu wa kuweka rangi ya bluu kwenye shati pamoja na viboksi.

"Hapo umemaliza, shati lilikuwa likifuliwa lazime litiwe bluu, sijui kama haya mambo bado yapo, dah. Mimi ndiyo nilikuwa nawapiga wasiojua, nilikula sana vipesa vyao kwa staili hii, "mchangiaji mwingine aliandika.

Yupo aliyetaja mpaka staili ya kutembea wakati denti akiwa amevaa shati lililowekwa viboksi na bluu.

"Unanyunyizia maji kidogo wakati wa kupiga vile ukitoka unahisi kama kila mtu anakuangalia wewe, na ukiona wanakuangalia sana unavunja bega."

Mwingine alidai kuwa staili ile ndiyo ilikuwa inaongoza kwa kumaliza mashati ya shule.

"Na usisahau ndiyo ilikua staili iliyokua inaongoza kwa kumaliza mashati ya shule, yaani yanachanika mgongoni, mikononi, na kwenye makwapa."

Kuna huyu aliyesema hayo hayo unarembesha na mhuri wa shule.

"Sisi tulikuwa tunaita kishada staili, mwenyewe umeweka na bluu yako, upande wa kushoto umerembesha na muhuri wa shule, yaani uko smati kabisa."

Denti mwingine wa zamani akasema hali ilivyozidi kuwa mbaya walimu wao wakapiga marufuku.

Hivi staili tulikuwa tukiita bati, ila baada ya hali kuzidi kuwa mbaya, ubitozi umezidi kuliko masomo, walimu walipiga marufuku."

**Tuma meseji 0716 350514**

MAKALA MAALUM

# Utekelezaji mikakati ya watoto Tanzania ulivyoikuna UNICEF

## • Kupungua maambukizo VVU, uandikishaji watoto shuleni waing'arisha nchi kimataifa

**Na Mwandishi Wetu**

NOVEMBA 20 kila mwaka huwa ni maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Haki za Watoto. Kwa Tanzania maadhimisho hayo mwaka huu yalifanyika kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam Novemba 29 mwaka huu.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan, alitumia fursa hiyo kuiomba Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuusambaza waraka wa adhabu za viboko shuleni wa mwaka 2002 ili walimu na wanafunzi wauelewe.

Dk. Dorothy anasema ukatili kwa watoto unaendana na kuudhuru mwili ikiwa ni pamoja na vipigo, ikijumuisha adhabu ya viboko vilivyopitiliza shuleni.

"Hivyo, viboko vilivyopitiliza ni ukatili kwa watoto kwa kuwa tunao Waraka na 24 wa Mwaka 2002 unaosimamia adhabu za viboko shuleni ambao unasema wazi ni nani mwenye mamlaka ya kutoa adhabu hiyo na viboko vingapi vinaruhusiwa na kwa utaratibu upi.

"Ninajua changamoto iliyopo ni usimamizi wa utekelezaji wa waraka huo, baadhi ya walimu hawaufuati wanapotoa adhabu, hawa walimu ninawataka wabadilike, vinginevyo sitamwacha mwalimu asishtakiwe kwa Sheria ya Mtoto iwapo atatoa adhabu hiyo nje ya waraka huo, sitamwacha," anaonya.

Waziri Dorothy anawahakikishia watoto kwamba timu ya serikali, wadau na jamii watakutana kuona namna nzuri ya kulishughulikia hoja ya viboko kwa kuzingatia maadili na tamaduni katika malezi.

"Inasikitisha kuona baadhi ya watoto wanaacha shule kwa sababu ya kukimbia viboko huku wengine wakipata majeraha makubwa na ulemavu na hata kupoteza maisha eti kwa sababu ya adhabu za viboko, hii haikubaliki kwani hii adhabu ya viboko haikulenga kusababisha mateso kwa watoto na ndiyo maana tunao waraka," anafafanua.

Dk. Dorothy anasema serikali itaziimarisha Kamati za Ulinzi wa Watoto na Wanawake na Madawati ya Ulinzi wa Watoto Shuleni ili waufahamu Waraka wa Viboko, hivyo kutotendwa kinyume na wakibaini kuwa ni kinyume, wapaze sauti haraka.

Waziri huyo pia anawaonya wanaume wanaolawiti na kunajisi watoto kuwa serikali haiwezi kuvumilia vitendo, hivyo sheria itaendelea kuchukuliwa dhidi ya wote watakaobainika.




Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) Shalini Bahuguna akizungumza wakati wa maadhimisho hayo, akiipongeza Tanzania kwa kupunguza vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima akifafanua jambo alipomwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Haki za Watoto jijini Dar es Salaam Novemba 29 mwaka huu.

Watoto walioshiriki maadhimisho hayo wanaeleza baadhi ya hoja zao kwa waziri ikiwamo kuomba marekebisho ya Sheria ya Ndoa, kupata huduma na taarifa sahihi kuhusu afya ya uzazi pamoja na kuondolewa kwa adhabu zinazodhuru mwili hasa viboko.

Viongozi wa dini hawako nyuma katika kuadhimisha siku hiyo. Katibu wa Baraza Kuu la Waislamu (BAKWATA), Shekh Nurdin anasema wanashirikiana na serikali katika kutoa maoni ya kurekebisha Sheria ya Ndoa ili kuwalinda watoto wa kike dhidi ya ndoa za utotoni.

Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF), Shalini Bahuguna anayatumia maadhimisho hayo kuipongeza Serikali ya Tanzania kwa kupunguza vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano na kusema Tanzania ni moja ya nchi zinazoongoza kwa kutekeleza programu za watoto.

Anakumbusha kuwa zaidi ya nusu ya Watanzania ni vijana, hivyo nchi itapata manufaa zaidi ikiwekeza kwenye kundi hilo na kuhakikisha inaungana na Umoja wa Mataifa (UN) kuliinua kundi hilo kiuchumi.

"Tunapoadhimisha Siku ya Kimataifa ya Haki za Watoto, tunakumbusha kwamba idadi ya watu Tanzania inaonyesha hadi mwaka 2020 nchini ilikuwa na watoto milioni 28 na idadi yao inakadiriwa kuongezeka maradufu hadi milioni 59 mwaka 2050. Hii inatukumbusha kwanini tunapaswa kuwekeza kwa watoto, ni kwa sababu wao ndiyo taifa letu lijalo.

"Tanzania bila shaka itatoka kuwa nchi ya uchumi wa chini kwenda uchumi wa juu, hatuna njia nyingine zaidi ya kuwekeza kwa watoto na kuwasikiliza watoto wetu wanataka nini.

"Nchi hii inapaswa kusherehekea kutokana na mafanikio makubwa iliyoyapata katika kupigania maendeleo ya watoto. Imepunguza sana vifo vya watoto walio chini ya umri wa miaka mitano.

"Vilevile, utapiamlo kwa watoto umepungua kwa takriban theluthi moja; maambukizi mapya ya VVU kwa watoto yamepungua kwa takribani asilimia 69; utoaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto walio na umri wa chini ya miaka mitano umeongeza na kufikia asilimia 65 mpaka mwezi Desemba mwaka jana kutoka asilimia 17 iliyokuwapo mwaka 2017

"Watoto zaidi wanaandikishwa shule za awali na shule ya msingi na kuifanya Tanzania kuwa nchi ya tatu Afrika kwa kuandikisha watoto zaidi shuleni," anabainisha.

Mwakilishi Mkazi wa UNICEF huyo anasema jambo la kufurahia zaidi ni kutolewa mwongozo wa elimu jumuishi, ukiwalenga watoto waliopata ujauzito shuleni na wale wenye ulemavu.

Vilevile, anapongeza mkakati wa serikali chini ya Rais Samia wa kuhakikisha hakutokei kifo cha uzazi kinachozuilika nchini, akihimiza nguvu ielekezwe pia kukabiliana na ukatili dhidi ya watoto wa kike na kiume.

"Watoto wapendwa, wasichana na wavulana, muwe na ndoto kubwa, mjue kuwa mna sauti na mtimize matarajio yenu. Tufanye kazi pamoja ili watoto wetu wa kike na wa kiume wafurahie haki zao na kutimiza matarajio yao.

"Hatuna muda wa kwenda polepole, tunahitaji kwenda haraka tukiwa na sera bora ili tuhakikishe watoto milioni 30 wa leo na watoto milioni 60 watakaokuwapo mwaka 2050, wote wanafurahi haki zao.

"Tuifanye Tanzania kuwa kinara wa haki za watoto katika ukanda huu, katika Bara la Afrika na duniani kote kwa ujumla," anahimiza Mwakilishi Mkazi wa UNICEF nchini.

# HADITHI


MAWENI ni moja kati ya vijiji nchini ambavyo vipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na kuwa vipo kilometa nyingi, miundombinu yake na mawasiliano yamekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa baadhi ya viongozi wa kijiji kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji, kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia. Badala yake wanakijiji wanalima kwenye ardhi aliyouziwa mwekezaji huyo. Mazao yaliyopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haiwatoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kunyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, ni mmoja wa wasichana warembo kijijini hapo ni mmoja waliopata shida hiyo. Hawana pa kupeleka malalamiko, wala wa kumlilia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.

# MTAKE MSITAKE-8

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

**MAWENI ni moja kati ya vijiji nchini ambavyo vipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na kuwa vipo kilometa nyingi, miundombinu yake na mawasiliano yamekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa baadhi ya viongozi wa kijiji kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji na kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia. Badala yake wanakijiji wanalima kwenye ardhi aliyouziwa mwekezaji huyo. Mazao yaliyopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haiwatoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kunyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, mmoja wa wasichana warembo kijiji hapo ni mmoja ya waliopata shida hiyo. Hawana kwa kupeleka malalamiko, wala wa kumlilia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.**

****************************************




Kijiji kiliamka na habari mpya. Ilikuwa ni ya kusikitisha kwa baadhi ya wanakijiji na baadhi ilikuwa ni kama sherehe.

"Kamwagiwa na Enock au na Mary?" Kijana mmoja aliwauliza wenzake aliokuwa amekaa nao chini ya mti wakicheza drafti.

"Kamwagiwa na Enock, si jamaa kajifanya kujipendekeza hadi kawa rafiki yake, kumbe anamchukulia mchumba wake, Enock akawafumania. Nasikia kamwagia maji ya betri machoni amekimbizwa kwenye hospitali ya mkoa. Akiona tena yule sijui."

Kijana mwingine akamtazama mwenzake, halafu akajibu. "Siyo hivyo nilivyosikia mimi. Ukweli ni kwamba jamaa kweli kamwagiwa sijui maji ya betri, sijui tindikali, lakini aliyemwagia ni Mary mwenyewe." Muulizaji na yule aliyeongea mara ya kwanza wote wakashtuka.

"Ndiyo, siyo kweli kwamba alikuwa mchumba wa Mary. Walikuwa marafiki tu wa kufahamiana na kuzoeana. Yule jamaa alimuokoa Mary kwenye ajali ya bodaboda. Haiwezekani mwanamke akawa na mpenzi halafu akaenda kumkutanisha na mchumba wake, wakawa marafiki, si kweli tunadanganyana. Hakuwa mpenzi wake, ila nasikia jamaa baadaye akawa na tamaa, akaanza kumtongoza. Kila akimkatalia, jamaa analazimisha tu, mwanamke akawa anamuelewesha kuwa wewe ni rafiki wa mchumba wangu haelewi, akaona hali hii siku moja tutakuja kufumwa. Hivi tu kuna baadhi ya watu wanatufikiria vibaya, je tukifumwa, kwa hasira akamwagia tindikali."

> **"Kijiji kina mambo hiki." Akasema huku akitikisa kichwa. Sauti yake iliwafanya wale vijana wawili kushtuka na kumtazama.**

Ilikuwa ni wakati huo huo msichana Ziada alikuwa anapita maeneo hayo na kuyasikia yote.

"Ai nyinyi wanaume wazima wambea, yaani mmekaa hapa mnazungumzia mambo ya watu. Halafu wote waongo. Tuulizeni sisi tunayoyajua ya chini ya uvungu."

"We unajua nini cha ziada?" Mmoja akauliza kwa namna ya kumkejeli.

"Wee, nyinyi hapa nimesikia mara Enock ndiyo kamwagia tindikali kamfumania, mara Mary kamwagia kwa sababu yule mwanaume kamtongoza, yaani mnababaisha tu. Kilichotokea sisi wa karibu ambacho tunakijua, ni Mary mwenyewe kafanya tukio hilo kwa sababu ya kuhofia kujulikana kama ana uhusiano naye.

Mchumba wake alipata taarifa kuwa anachukuliwa mwanamke na huyo rafiki yake, akaweka mtego, Mary akaona ili awe salama nimwagie tu tindikali ili ionekane ametongozwa, lakini yeye hamtaki na amesumbuliwa mpaka amefanya hivyo. Ukweli Mary pale kaua soo." Ziada akamaliza umbea wake akapita na ndoo yake ya maji aliyokuwa ameibeba, akatokea kijana mwingine anayeitwa Nanje. Alikuwa akisukuma mkokoteni wake.

"Kijiji kina mambo hiki." Akasema huku akitikisa kichwa. Sauti yake iliwafanya wale vijana wawili kushtuka na kumtazama.

"Nanje nini tena?" Mmoja akauliza. Nanje akasimamisha mkokoteni wake. Ilionekana kabisa kuwa moyoni mwake ana dukuduku ambalo anataka kulisema.

"Haya mambo kwenye kijiji hiki kila kukicha kunazuka jambo jipya yataisha lini?" Akajifanya kuuliza. Hakukuwa na jibu. Akajijibu mwenyewe.

"Kijana wa watu mgeni wamemwagia tindikali, sijui kama ataona tena. Yaani mapenzi haya! Hivi mtu kama ukikataliwa si ukubali tu."

"We Nanje unatuzingua bwana, unaongea mafumbo mafumbo, nani sasa akubali?" mcheza drafti mwingine akauliza. Nanje akasogea karibu, akaangalia huku na huku, halafu akaongea kwa sauti ya chini. "Usonzo." Wote wakashtuka.

Hawakutegemea kama atatajwa mtu huyo. Habari iliyopo kijiji ni kwamba Adel amemwagiwa tindikali. Wengine wanasema ni Enock na wengine ni Mary. Na sababu zimetajwa hapo. Sasa hii mpya ya mwekezaji Mosha Usonzo kuhusika lilikuwa ni jambo jipya kabisa.

"Wote wanababaisha tu hapa kijijini, hakuna la ukweli hata kidogo zaidi ya hili ninalowaambia mimi. Usonzo katuma kikosi chake cha kazi kumwagia Adel tindikali. Kisa anamtaka msichana Mary muda mrefu tu. Kabla hata kijana wa watu hajaja, nyinyi wenyewe mnalijua hili. Na yule tajiri anaweza kufanya jambo lolote. Kijana wa watu kaja juzi juzi tu kaopoa mzigo, yeye na mipesa yake kaambulia mineno ya shombo. We unafikiri mkubwa kama yule keshanunua kijiji kizima hiki wote tuko chini yake atafanya nini?" Kamwagia kwa kumkomoa kijana wa watu hana baya yule, sijawahi kusikia kagombana na mtu tangu kaingia kijiji hiki."

Kulikuwa na habari nyingi tofauti, kila mmoja akisema lake. Kila mmoja kidai analosimua yeye ni sahihi kiasi cha kuwachanganya wapokeaji wasijue ukweli ni upi.

Kama kawaida ya maneno ya kusikia kila anayepokea na kwenda kulisimulia kwa mwingine ni lazima kitiwe chumvi lai kidogo ili kunomnogesha anayeambiwa.

Vyovyote itakavyokuwa ukweli ukabaki pale pale kuwa Adel amemwagiwa kitindikali machoni na amelazwa kwenye hospitali ya mkoa, hali yake ilielezwa kuwa ni mbaya sana. Hata hivyo hakuna yoyote ambaye ametajwa kufanya tukio hilo, kutaja mahali alipomwagiwa. Madaktari hawajasema lolote, lakini uvumi unasema kuwa huenda akawa haoni tena, au akapoteza macho yake.

Ingawa alikuwa mgeni lakini hali ya taharuki ilionekana kijijini hapo, hasa ikizingatiwa wanaodaiwa kufanya hivyo ni wanakijiji.

Wa kwanza ni Mary, wa pili Enock ambaye ni mchumba wa Mary na wa tatu ni Usonzo, tajiri mwekezaji ambaye naye amekufa na kuoza kwa binti wa watu Mary.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# POLISI TANZANIA YAIPANIA AZAM, YAMWAJIRI ZAHERA

**Hadija Mngwai na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupata kichapo cha mabao 3-1 kutoka kwa Simba, mabosi wa Polisi Tanzania wamesema timu yao haitarudia makosa na imejipanga imara kuhakikisha inapata ushindi katika mechi yao dhidi ya Azam FC.

Polisi Tanzania inatarajia kuikaribisha Azam FC katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa Jumatatu kwenye Uwanja wa Ushirika ulioko Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Maafande hao ndio wanaburuza mkia kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Polisi Tanzania, Frank Lukwaro, alisema timu yao iko katika nafasi mbaya na wanatakiwa kupambana kwenye mechi hiyo na kurejesha matumaini ya ushindani.

**Juma alisema wamejipanga kurekebisha makosa na hatimaye kujiondoa katika eneo hilo la hatari kwa kuzibakisha pointi zote tatu watakapoikaribisha Azam.**

"Tunahitaji ushindi dhidi ya Azam FC, iwe jua, iwe mvua, ushindi ni muhimu ili tujikwamue kutoka katika nafasi ya mkiani. Tutapambana kuzibakisha alama tatu, tunaimani kabisa tutazipata kwa sababu mahali tulipo hivi sasa ni hatarishi, taa nyekundu imeshawaka, ni mahali hatari kwetu," alisema Juma.

Aliongeza mechi hiyo inatarajiwa kuwa na ushindani kwa sababu Azam anahitaji ushindi ili kujiimarisha kwenye msimamo na kuendelea kuwamo katika mbio za kuwania ubingwa.

"Mchezo huu utakuwa wa kipekee kabisa, panyeshe mvua, pavuje ama kuwe na jua pointi tatu muhimu, hatuhitaji kupoteza mechi hii," aliongeza.

Wakati huo huo, Polisi Tanzania imemtambulisha rasmi aliyekuwa Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, kuwa kocha wake mpya.

Lukwaro imesema klabu hiyo imemtwaa Mkongomani huyo baada ya kukamilisha mazungumzo ya muda mrefu yaliyokuwa yanaendelea baina ya pande hizo mbili.

Mechi hiyo inatarajiwa kukamilisha mzunguko wa kwanza na baada ya hapo mechi za mashindano ya Kombe la FA, hatua ya pili zitaendelea.




Mkurugenzi wa Kampuni ya Parimatch Tanzania, Erick Gerald (kulia) akikabidhi kadi ya pikipiki kwa mshindi wa wiki wa promosheni ya michuano ya Kombe la Dunia ya 'Chomoka na Ndinga', Elikisai Samuel. Kushoto ni Ofisa Masoko wa Kampuni ya Hero, Norah Mapunda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Chomoka na Ndinga yaendelea

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya michezo ya kubahatisha ya Parimatch Tanzania imewatangaza rasmi washindi wawili watakaopata zawadi ya pikipiki kutoka katika promosheni ya kila wiki ya 'Chomoka na Ndinga' inayohusisha wateja wake katika michuano ya Kombe la Dunia inayoendelea nchini Qatar.

Mkurugenzi wa Parimatch Tanzania, Erick Gerald, aliwataja washindi hao ni Elikisai Samuel wa Dar es Salaam na Elgilius Willbroad wa mkoani Kagera ambao wamejishindia bodaboda aina ya Hero Hunter 125cc yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 1.5 kila moja.

Mbali na bodaboda hizo, kampuni hiyo pia ilitoa zawadi ya simu aina ya Samsung Galaxy A03 Core kwa washindi 10, washindi wawili hupatikana kila siku.

Naye Ofisa Habari wa Parimatch Tanzania, Ismael Mohamed, alisema promosheni hiyo ni mahususi kwa wateja wote wenye akaunti na hata wateja wapya watakaojiunga katika kipindi hiki cha Kombe la Dunia.

"Katika kipindi cha kuanzia 22.11.2022 hadi 26.12.2022, mteja wa Parimatch akifanya bashiri kwenye mchezo wowote basi ataingia moja kwa moja katika droo ya kuwania gari mpya aina ya Urban Cruiser, bodaboda aina ya Hero Hunter 125cc na smartphone aina ya Samsung Galaxy A03 Core," alisema Mohamed.

Aidha Mohamed aliendelea kwa kusema kuwa kila siku watakuwa wanatoa simu mbili (2) na washindi watakuwa wanatangazwa kupitia kurasa zao za kijamii na zawadi ya bodaboda itatolewa kwa wiki mara moja, siku ya Ijumaa, kupitia droo itakayoruka kituo cha ITV wiki husika.

Zawadi ya gari itatolewa mwisho wa mashindano haya Desemba 27 ambapo droo kubwa ya kutafuta mshindi wa gari itafanyika siku hiyo.

## Sare yamvuruga kocha Mbeya City

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Mbeya City, Abdallah Mubiru, amewajia juu wachezaji wake baada ya mechi ya juzi dhidi ya KMC akisema walicheza chini ya kiwango huku akiwashangaa kwa kitendo cha kufurahia matokeo ya sare.

Mubiru, Kocha wa zamani wa Vipers, KCCA zote za Uganda, alisema hakufurahishwa na namna kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, na kumalizika timu hizo zikifungana bao 1-1.

"Nawapongeza KMC wamecheza vizuri, walikuwa na plani nzuri katika mechi hiyo, lakini sikufurahishwa kabisa na uchezaji wa wachezaji wangu, Nimeshangaa kuona timu ndogo wakipata sare ugenini wanashangilia. Unashangiliaje sare?" alilalamika kocha huyo.

Naye Kocha Mkuu wa KMC, Thierry Hitimana, aliendelea kulia na majeruhi ndani ya kikosi chake, lakini kwa safari hii akaongeza ugumu wa ratiba umechangia timu hiyo kupata matokeo yasiyofurahisha.

Sare katika mechi hiyo ilifanya Mbeya City kumaliza mzunguko wa kwanza na pointi 20 mkonini wakati KMC FC wao wamefikisha pointi 16.

## Singida Big Stars yaruhusiwa kusajili wapya

**Na Adam Fungamwango**

KAMATI ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), imeiondolea Singida Big Stars adhabu ya kutosajili nyota wapya katika kipindi cha dirisha dogo la usajili linalotarajiwa kufunguliwa Desemba 15, mwaka huu.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Clifford Ndimbo, alisema badala yake kutumikia adhabu hiyo, Singida Big Stars sasa watatakiwa kulipa faini ya Sh. milioni moja kutokana na kosa lililokuwa linawakabili.

Ndimbo alisema uamuzi huo umefanywa na kamati hiyo baada ya kuipitia hoja za Singida Big Stars na kuongeza endapo itashindwa kulipa faini hiyo ndani ya muda, adhabu hiyo itabaki pale pale.

Oktoba mwaka huu, kamati hiyo ilizifungia klabu za Singida Big Stars na Prisons kwa kubainika kusajili wachezaji ambao wana mikataba na timu zingine.

Wakati Prisons ikimsajili kipa, Mussa Mbisa aliyekuwa na mkataba wa Coastal Union, Singida Big Stars ilimsajili Metacha Mnata aliyekuwa bado ana mkataba na Polisi Tanzania.

## ZISIKUPITE

### JOAO AWEKWA SOKONI
KLABU ya Atletico Madrid itakuwa tayari kumuuza, Joao Felix kwa euro milioni 100 baada ya kumsajili fowadi huyo wa Timu ya Taifa ya Ureno mwenye umri wa miaka 23 kwa euro milioni 126 mwaka wa 2019. ***(AS)***

### MAN NAO WAMTAKA
MANCHESTER United ina nia ya kutaka kumsajili Joao Felix, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Paris St-Germain na Bayern Munich katika jitihada za kumnunua Januari. ***(Mail)***

### MESSI, PSG BADO SANA
KLABU ya PSG pia itampa mshambuliaji na nahodha wa Timu ya Taifa ya Argentina, Lionel Messi, mwenye umri wa miaka 35 nyongeza ya mkataba mpya baada ya Kombe la Dunia. ***(Goal)***

### AL HILAL WAMTAKA RONALDO
AL Hilal wanataka kuwashinda wapinzani wao wa Saudi Arabia, Al-Nassr katika kumsajili Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37 baada ya mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Ureno kuondoka Manchester United. ***(Express)***

### CHELSEA YAMWANIA GVARDIOL
CHELSEA inabakia kwenye mazungumzo na RB Leipzig kuhusu kumsajili, Josko Gvardiol, na beki huyo wa Timu ya Taifa ya Croatia mwenye umri wa miaka 20, amesema "labda siku moja nitakuwepo". ***(Atheletic via 90 min)***

### SOYUNCU ATAJWA ATLETICO
KLABU ya Atletico Madrid imefanya uchunguzi kuhusu kiungo wa kati wa Leicester na Timu ya Taifa ya Uturuki, Caglar Soyuncu, mwenye umri wa miaka 26. ***(AS)***

### LIVERPOOL NA BELLINGHAM
MKURUGENZI Mtendaji wa Borussia Dortmund, Carsten Cramer, amesema wana "uhusiano mzuri" na Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp, lakini hawatapata "upendeleo" wowote kama wanataka kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19 kutoka klabu hiyo ya Ujerumani. . ***(Vietnam News)***


### RICE KUONDOKA WEST HAM
KIUNGO wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 23 ameashiria anataka kuondoka West Ham, akisema anahitaji kushinda mataji na kucheza mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Guardian)***

### SCARPA ABUKIA FOREST
KLABU ya Nottingham Forest imefikia makubaliano ya kumsajili kiungo mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Brazil, Gustavo Scarpa mwenye umri wa miaka 28 kutoka Palmeiras. ***(Fabrizio Romano)***

### SANTOS AGOMBEWA EPL
CHELSEA inashindana na Newcastle United kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Brazil, Andrey Santos, mwenye umri wa miaka 18 kutoka Vasco da Gama. ***(90 min)***

### KESSIE AICHOKA BARCA
MCHEZAJI wa Barcelona aliyesajiliwa majira ya joto, Franck Kessie mwenye umri wa miaka 25 ambaye ni raia wa Ivory Coast hajisikii vizuri ndani ya klabu hiyo. ***(AS)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MULLER ADOKEZA NIA YA KUSTAAFU

●●● Ni baada ya mshambuliaji huyo kutoa kauli tata Ujerumani ikicheza mechi yake...

**DOHA, Qatar**

THOMAS Muller amekiri hajui kama ameichezea Ujerumani mechi yake ya mwisho baada ya kuondolewa kwenye Kombe la Dunia la 2022 katika hatua ya makundi.

Ujerumani ilihitaji Japan ifungwe na Hispania ili kupata matumaini ya kufuzu katika mechi ya juzi, lakini ushindi wa kushangaza wa magoli 2-1 kwa Samurai wa Bluu hao ulifanya ushindi wake wa mabao 4-2 dhidi ya Costa Rica usiwe na maana yoyote.

Baada ya mchezo huo, Muller alitoa kauli ambayo mashabiki wengi wanahofia inaweza kuwa ya kwaheri.

"Ni janga kabisa," alisema Muller akiwaambia waandishi wa habari. "Sijui jinsi ya kusonga mbele.

"Ikiwa huo ulikuwa mchezo wangu wa mwisho, basi ningependa kusema maneno machache kwa mashabiki wa soka wa Ujerumani. Ilikuwa ni furaha kubwa. Asanteni sana. Siku zote nilijaribu kuonyesha moyo uwanjani. Kitu ambacho kilikuwa machozi ya furaha.

"Ninahitaji kufikiria juu ya kila kitu sasa."

Muller yuko katika nafasi ya saba kwenye orodha ya wafungaji bora wa muda wote wa Ujerumani akiwa amepachika wavuni mabao 44.

Tangu aichezee kwa mara ya kwanza Ujerumani mwaka 2010, Muller amecheza mechi 120 na alikuwa sehemu muhimu ya kikosi kilichoshinda taji la Kombe la Dunia mwaka 2014, fainali zikifanyika nchini Brazil.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,054,9

MECHI KALI

COASTAL UNION
VERSUS
SIMBA

1 | 6.24
X | 3.66
2 | 1.50

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa airtel money


SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# BUSQUETS: HATUJAIKWEPA BRAZIL



**DOHA, Qatar**

SERGIO Busquets alikanusha maoni kuhusiana na Hispania kuwa ilifarijika kwa kukwepa mchezo wa hatua ya mtoano wa timu 16 wa Kombe la Dunia dhidi ya Brazil baada ya La Roja hao kushika nafasi ya pili katika Kundi E.

Hispania walikuwa kwenye mstari wa kuongoza kundi wakati Alvaro Morata alipowapa uongozi wa mapema dhidi ya Japan kwenye Uwanja wa Khalifa Alhamisi, lakini Ao Tanaka na Ritsu Doan walifunga mabao ndani ya sekunde 142 na kuwafunga Samurai wa Bluu hao na kupanda hadi nafasi ya kwanza.

Kipigo cha Hispania kiliwafanya wasonge mbele kwa tofauti ya mabao huku Ujerumani ikiilaza Costa Rica magoli 4-2 katika mchezo mwingine wa kundi hilo.

Hispania sasa itakutana na Morocco katika hatua ya 16 bora, na endapo Brazil haikupoteza dhidi ya Cameroon jana Ijumaa, hawataweza kukutana na timu zinazopigiwa upatu kabla ya mechi hiyo hadi fainali.

Hata hivyo, Busquets alikanusha alipoulizwa kama hiyo iliwakilisha matokeo chanya, akisema: "Haina uhusiano wowote nayo.

"Tulitaka kushinda na kuwa wa kwanza. Tunaenda upande wa pili wa mabano, lakini hiyo haihakikishi itakuwa rahisi au ngumu zaidi.

"Hatukutaka hili litokee, nia yetu ilikuwa ni kushinda, ili kuendelea, tuna hatua ya 16 bora dhidi ya Morocco, mechi ambayo itakuwa ngumu sana.

"Hatukuwa na raha. Walifunga pasi kati ya mistari vizuri sana na ilikuwa ngumu sana kwetu kuunganisha na kuunda hatari.

# Pulisic kuwa fiti kuivaa Uholanzi leo

**DOHA, Qatar**

CHRISTIAN Pulisic amesema atafanya kila awezalo ili kuwa fiti kwa ajili ya mechi ya hatua ya 16 bora ya Kombe la Dunia itakayowakutanisha Wamarekani dhidi ya Uholanzi, leo.

Pulisic alipata jeraha la alipofunga bao la ushindi katika ushindi wa Marekani dhidi ya Iran, Jumanne.

Fowadi huyo wa Chelsea alitolewa wakati wa mapumziko, lakini anatumaini atakuwa fiti kwa wakati ili kukabiliana na Uholanzi kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Khalifa wikendi hii.

Pulisic wakati wa mkutano na waandishi wa habari Alhamisi alisema, "hivyo ndivyo itakavyokuwa, lakini nadhani nitakuwa sawa.

Mchezaji huyo wa zamani wa Borussia Dortmund amedhamiria kutimiza wajibu wake kwa Marekani itakapokwenda kutafuta nafasi ya kutinga robo fainali.

"Ona tu jinsi ninavyojisikia, nikichukulia siku baada ya siku hivi sasa. Lakini nitafanya kila niwezalo kurejea uwanjani Jumamosi.



## HABARI MICHEZO


938,985/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 03/12/22 | 18:00 | Accrington vs Oxford Utd | 3.08 | 3.42 | 2.23 |
| 2. 03/12/22 | 18:00 | Northampton vs Tranmere | 2.25 | 3.18 | 3.28 |
| 3. 03/12/22 | 18:00 | Cove Rangers vs Partick Thistle | 2.78 | 3.53 | 2.37 |
| 4. 03/12/22 | 18:00 | Arbroath vs Morton | 2.59 | 3.24 | 2.69 |
| 5. 03/12/22 | 19:00 | Sakaryaspor vs Erzurum BB | 2.30 | 3.48 | 2.88 |
| 6. 03/12/22 | 20:00 | Cagliari vs Parma FC | 2.43 | 3.19 | 2.94 |
| 7. 03/12/22 | 20:30 | Mirandes vs Albacete Balompie | 2.50 | 3.06 | 2.96 |
| 8. 03/12/22 | 20:30 | Sporting Gijon vs Las Palmas UD | 2.64 | 3.04 | 2.79 |
| 9. 03/12/22 | 21:00 | Deportivo La Coruna vs Cordoba | 2.26 | 3.02 | 3.02 |
| 10. 03/12/22 | 23:00 | Villarreal B vs Leganes | 2.45 | 3.02 | 3.07 |
| 11. 04/12/22 | 13:30 | Manisa BBSK vs Keciorengucu | 2.34 | 3.46 | 2.82 |
| 12. 04/12/22 | 14:30 | Spal vs Modena | 2.33 | 3.12 | 3.17 |
| 13. 04/12/22 | 15:30 | Wycombe vs Portsmouth | 2.42 | 3.39 | 2.79 |
| 14. 04/12/22 | 16:00 | Adanaspor vs Goeztepe | 2.63 | 3.38 | 2.53 |
| 15. 04/12/22 | 17:00 | Sudtirol vs Frosinone | 3.37 | 3.03 | 2.28 |
| 16. 04/12/22 | 17:00 | Cosenza vs Perugia | 2.94 | 3.09 | 2.49 |
| 17. 04/12/22 | 17:00 | Brescia vs Reggio Calabria | 2.54 | 2.98 | 2.98 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 03/12/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 1197 | Bodrumspor vs Genclerbirligi | 1.40 | 4.28 | 6.61 |
| 14:45 | 2680 | Apollon Smyrnis vs Kissamikos | 1.65 | 3.30 | 5.24 |
| 15:00 | 1892 | Ulinzi Stars vs Posta Rangers | 2.18 | 2.85 | 3.85 |
| 15:00 | 1941 | Mornar Bar vs Buducnost | 4.18 | 3.21 | 1.82 |
| 15:00 | 2466 | Dila Gori vs FC Samgurali Tskaltubo | 1.31 | 4.47 | 8.75 |
| 15:00 | 5233 | Chennaiyin FC vs Hyderabad FC | 3.65 | 3.45 | 1.87 |
| 15:15 | 2780 | AL Tadamon Sour vs Shabab AL Sahel | 2.60 | 3.15 | 2.70 |
| 15:30 | 1114 | Shrewsbury vs Lincoln | 2.22 | 3.18 | 3.18 |
| 15:30 | 3267 | AFC Wimbledon vs Grimsby | 2.93 | 3.18 | 2.36 |
| 15:30 | 3827 | Derby vs Sheffield Wed | 3.03 | 3.27 | 2.25 |
| 15:30 | 5166 | Sunderland vs Millwall | 2.46 | 3.16 | 2.81 |
| 15:30 | 5512 | Scunthorpe vs Notts County | 8.10 | 5.14 | 1.30 |
| 15:30 | 5729 | NK Dugopolje vs Orijent Rijeka | 1.87 | 3.31 | 3.80 |
| 16:00 | 1121 | Forest Green vs Cambridge Utd | 2.54 | 3.19 | 2.69 |
| 16:00 | 3228 | Samsunspor vs Denizlispor | 1.33 | 4.68 | 7.60 |
| 16:00 | 3355 | Venezia vs Ternana | 2.34 | 3.17 | 2.97 |
| 16:00 | 3697 | Coastal Union vs Simba | 6.24 | 3.66 | 1.50 |
| 16:00 | 4156 | AS Kigali vs Kiyovu Sports | 2.48 | 2.73 | 3.02 |
| 16:00 | 4890 | Dodoma FC vs Ruvu Shooting | 1.93 | 2.96 | 4.08 |
| 16:00 | 5138 | Zanaco vs FC Muza | 1.85 | 2.97 | 4.48 |
| 16:00 | 5955 | Kariobangi Sharks vs Mathare United | 1.58 | 3.80 | 5.80 |
| 17:00 | 2305 | USM Alger vs ES Setif | 1.99 | 3.02 | 3.75 |
| 17:00 | 2358 | CR Belouizdad vs MC Alger | 1.71 | 3.21 | 4.87 |
| 17:00 | 3737 | Arsenal W vs Everton W | 1.11 | 7.57 | 15.53 |
| 17:00 | 5720 | Bengaluru FC vs ATK Mohun Bagan | 3.31 | 3.41 | 1.98 |
| 18:00 | 1215 | Queens Park vs Hamilton | 1.84 | 3.64 | 3.74 |
| 18:00 | 1321 | Rochdale vs Harrogate | 2.30 | 3.31 | 2.91 |
| 18:00 | 1667 | Cove Rangers vs Partick Thisle | 2.51 | 3.45 | 2.51 |
| 18:00 | 2288 | Ayr United vs Raith Rovers | 2.06 | 3.41 | 3.26 |
| 18:00 | 2459 | Ards FC vs Institute | 1.87 | 3.80 | 3.31 |
| 18:00 | 2539 | Inverness vs Dundee FC | 3.26 | 3.36 | 2.08 |
| 18:00 | 2564 | Stranraer vs Stirling | 3.07 | 3.46 | 2.06 |
| 18:00 | 3188 | Netherlands vs USA | 1.87 | 3.35 | 4.21 |
| 18:00 | 3206 | Northampton vs Tranmere | 2.62 | 3.02 | 2.72 |
| 18:00 | 3283 | Arbroath vs Morton | 2.56 | 3.15 | 2.66 |
| 18:00 | 3896 | ST Josephs FC vs Lynx FC | 1.45 | 4.57 | 5.25 |
| 18:00 | 3965 | Ballymena Utd vs Cliftonville Belfast | 4.46 | 3.88 | 1.62 |
| 18:00 | 4551 | Dunfermline vs Queen of South | 1.73 | 3.75 | 4.14 |
| 18:00 | 4575 | Linfield Belfast vs Carrick Rangers | 1.34 | 4.85 | 6.79 |
| 18:00 | 4603 | Accrington vs Oxford Utd | 3.07 | 3.42 | 2.17 |
| 18:00 | 5184 | Falkirk FC vs Airdrieonians | 2.01 | 3.40 | 3.40 |
| 20:00 | 1823 | Casa Pia Atletico vs Sporting Braga | 4.49 | 3.94 | 1.69 |
| 20:00 | 3832 | Cagliari vs Parma | 2.34 | 3.16 | 2.97 |
| 20:00 | 5334 | Pafos FC vs Olympiakos Nicosia | 1.33 | 4.90 | 8.80 |
| 20:30 | 2430 | Sporting Gijon vs Las Palmas UD | 2.67 | 2.96 | 2.72 |
| 20:30 | 3452 | Mirandes vs Albacete Balompie | 2.64 | 2.98 | 2.74 |
| 21:00 | 2429 | Deportivo La Coruna vs Cordoba | 1.92 | 3.20 | 3.74 |
| 22:00 | 5709 | Argentina vs Australia | 1.19 | 6.19 | 14.98 |
| 23:00 | 3272 | Villarreal B vs Leganes | 2.48 | 2.88 | 3.03 |
| 23:45 | 1210 | CD Trofense vs Pacos Ferreira | 3.19 | 3.49 | 2.13 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# COSOTA YATAKIWA KUFUNGUA 'MILANGO' KWA WADAU WOTE

**Na Saada Akida**

TAASISI ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) imetakiwa isiwe kama kisiwa kwa kukataa kushirikiana na taasisi nyingine za kiserikali zinazojihusisha na teknolojia ili kuimarisha ukusanyaji wa taarifa za matumizi ya kazi za sanaa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, wakati alipotembelea banda la Cosota, Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia, Kundo Mathew, alisema lengo la kufanya hivyo ni kuwasaidia wasanii wapate haki zao, fedha na fursa zozote zinazohusiana na kazi zao.

Kundo alisema kazi data zinazohusu kazi za wasanii inasaidia serikali kupata taarifa sahihi na ukusanyaji wa mapato kwa kufahamu sanaa inaingiza kiasi gani cha fedha.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Nikison Simon, 'Nikki wa Pili' alisema kongamano hilo ni muhimu kwa sababu linaangazia kuboresha mazingira ya wasanii na wabunifu.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Cosota, Doreen Sinare, alisema wamewakaribisha taasisi ya sheria ya ABC kutoa elimu ya kisheria kwa wasanii kufahamu namna wanavyoweza kulinda kazi na mikataba wanayoingia.



Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa (katikati), akikabidhi bendera ya Taifa kwa washindi wa shindano la 'Twenzetu Qatar na Hicence', kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere, Dar es Salaam juzi. Kushoto kwa waziri ni Ofisa Mkuu wa Tigopesa, Angelica Pesha. **PICHA : MPIGAPICHA WETU**

# Nabi afungiwa

INATOKA UK. 32

heshimu kwa sababu tulipoteza mechi iliyopota dhidi ya Ihefu FC kwa sababu hatukuwa makini, uchovu ulichangia.

Malengo yetu ni kuona tunafanya vizuri na kutetea mataji yetu, hatuwezi kufikia malengo yetu bila ya kujituma na kushinda mechi zote za Ligi Kuu pamoja na mechi za Kombe la Shirikisho la Azam," kocha huyo alisema.

Baada ya mechi ya kesho, Yanga itaenda ugenini Lindi kuwafuata Namungo FC hapo Desemba 7, mwaka huu halafu itarejea kuaanza kampeni ya kutetea taji la Kombe la FA kwa kuwakaribisha Kurungezi FC siku mbili baadaye na itawaalika Polisi Tanzania na Coastal Union kati ya Desemba 17 na 20, mwaka huu.

Vinara hao watakutana na Azam FC kwenye Uwanja wa Azam Complex halafu itakwenda Manungu Turiani kuwafuata wenyeji Mtibwa Sugar.

Katika hatua nyingine Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kupitia mtandao rasmi imetaja orodha ya timu tano zinazoshikilia rekodi ya 'Unbeaten' Afrika na kusema Yanga iko katika nafasi ya nne.

# MGUNDA AWAAMBIA

INATOKA UK. 32

ozoea uwanjani.

Chipo alisema mechi dhidi ya Dodoma Jiji ambayo timu yake ikiwa nyumbani ilifungwa bao 1-0 ilikuwa na mfumo tofauti na ule ambao anatarajia kuucheza leo atakapoikabili Simba.

"Tumejiandaa na mechi dhidi ya Simba, tulipoteza mechi iliyopita, lakini makosa tumeyarekebisha, tuko tayari kupambana, kila mechi ina mifumo yake, ni mechi mbili tofauti, mtaona vitu tofauti uwanjani," alisema Chipo ambaye alichukua mikoba ya Mgunda baada ya kuondoka kwa Wagosi wa Kaya.

Alisema tatizo lao kubwa Coastal Union ni sehemu ya ulinzi, lakini hana wasiwasi na safu yake ya ushambuliaji.

"Tahadhari kubwa itakuwa ni sehemu ya uzuiaji, wanatakiwa kuwa makini wakati wanapokuwa hawana mpira," Chipo aliongeza.

Ligi hiyo inatarajia kuendelea tena kesho kwa mabingwa watetezi kuwakaribisha Prisons kwenye Uwanja wa Taifa, Dar es Salaam.

# Michezo

Jumamosi Desemba 3, 2022

Nipashe




UKURASA 29

**Muller adokeza nia ya kustaafu**



Mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Croatia, Luka Modric (wa mbele), akiwania mpira dhidi ya nyota wa Ubelgiji, Jan Vertonghen katika mechi ya Kombe la Dunia ya Kundi F iliyochezwa kwenye Uwanja wa Ahmad Bin Ali Stadium jijini Al Rayyan, Qatar juzi usiku. Timu hizo zilitoka suluhu. **PICHA: MTANDAO**

# MGUNDA AWAAMBIA COASTAL WAJIPANGE

## ●●●Afunguka Simba imefuata ushindi Mkwakwani ingawa amekiri mechi hiyo...

**Na Adam Fungamwango**

MBIO za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara zinatarajia kuendelea tena kwa Coastal Union kuikaribisha Simba leo kwenye Uwanja wa CCM, Mkwakwani huku Kocha Mkuu wa Wekundu wa Msimbazi, Juma Mgunda akirejea nyumbani Tanga kwa mara ya kwanza tangu alipoachana na wenyeji hao.

Simba itashuka katika mchezo huo ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 3-1 walioupata dhidi ya Polisi Tanzania Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Ushirika ulioko Moshi, mkoani Kilimanjaro, wakati Coastal Union ilipoteza dhidi ya Dodoma Jiji.

Simba inahitaji kupata pointi tatu kwa udi na uvumba hasa baada ya watani zao wa jadi, Yanga kupunguzwa kasi waliporuhusu kufungwa mabao 2-1 na Ihefu.

Mnyama anaingia uwanjani leo akiwa kwenye nafasi ya tatu na pointi 31 mkononi huku Coastal Union yenye pointi 12 iko katika nafasi ya 12.

Zilipokutana msimu uliopita kwenye uwanja huo mechi ya mzunguko wa pili, Simba ilishinda mabao 2-1 na walipocheza mechi ya mwaka kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, timu hizo zilitoka suluhu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mgunda alisema maandalizi yote ya kuelekea katika mechi hiyo dhidi ya timu yake ya zamani yamekamilika na anaamini Simba itaibuka na ushindi.

"Nataka niseme jambo moja, tunacheza dhidi ya Coastal Union, maandalizi tumeshayafanya, tunaiheshimu Coastal ni timu nzuri na mimi nikiwa ni muasisi wa timu hiyo. Mimi ni Coastal Union na nimeichezea kwa muda mrefu, hata nilipokwenda kucheza soka la kulipwa nje ya nchi, niliporejea nchini nilibaki Coastal.

Nikamalizia soka langu hapo na hata nilipoanza kufundisha mpira nilianza kufundishia hapo hapo. Kwa sasa nipo Simba ndio kwenye kazi na ajira yangu, kwenye mechi hii nitakuwa natimiza wajibu wangu kama mwalimu wa timu ya Simba," alisema Mgunda.

Kocha huyo alisema amewasili Tanga na kikosi cha wachezaji 22 na anashukuru nyota waliokuwa majeruhi akiwamo Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' wameshapona na wamerejea kwenye hali ya kawaida.

Kocha Mkuu wa Coastal Union, Mkenya Yusuph Chipo, alisema katika mechi ya leo mashabiki wataona vitu tofauti na walivy-

INAENDELEA UK. 31

## Nabi afungiwa 3, akifikiria pointi 18

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, akifungiwa mechi tatu na kupigwa faini ya Sh. 500,000, mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wamesema wanahitaji kuvuna pointi 18 kutoka kwenye mechi sita watakazocheza Desemba hii.

Nabi amefungiwa na Kamati ya Uendeshaji ya Ligi Kuu kutokana na kukutwa na hatia ya kuwashambulia waamuzi baada ya kuonyeshwa kadi ya njano wakati Yanga ilipokuwa ugenini Mbarali, mkoani Mbeya, nyumbani kwa Ihefu SC.

Kampeni hiyo inatarajia kuanza kesho watakapoikaribisha Tanzania Prisons kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Nabi aliliambia gazeti hili tayari amefanya maboresho katika kikosi chake ili kuhakikisha wanarejea kwenye kasi yao ya ushindi kwa ajili ya kufikia malengo waliyowekwa mwezi huu.

Kocha huyo alisema ameendelea kuwakumbusha wachezaji wake kupambana ili kupata ushindi katika kila mechi na hatimaye kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi hiyo inayotoa tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Alisema amezidi kuwapa mbinu washambuliaji wake ili waongeze umakini wanapoingia katika eneo la hatari la mpinzani na kumalizia kazi nzuri iliyotangulia na kutengeneza nafasi hiyo ya kufunga.

"Ni makosa ya kibinadamu huwa yanajitokeza, kikubwa tunakumbushana tu ili kupunguza makosa yanayozuilika, tunahitaji kutafuta matokeo chanya katika hii michezo yetu ya mwezi huu kwa kukusanya pointi 13 kabla ya kuanza mwaka mwingine," alisema Nabi.

Mtunisia huyo alisema kwa sasa anahitaji alama tatu katika mechi dhidi ya Tanzania Prisons na anaimani mchezo huo utakuwa na ushindani kwa sababu wapinzani wana timu nzuri na inacheza vyema.

"Hatuwadharau Tanzania Prisons, ni timu inayocheza vizuri, nimezungumza na wachezaji wangu wawe makini na kuwa-

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >